

MASWALI NA MAJIBU

 Ndugu Beeler, una ujumbe kwa ajili ya usiku huu? Ni—nimepwewa sauti kidogo. Nilikuwa ningali na—na maswali kadha. Kama hawa... Kama mmoja wa ndugu hawa angechukua na kuhubiri, ningefurahi. Sasa, msichochewe. Hii si... Hizi ni nguo za kuombewa zinazoenda kule Afrika. Hiki chote kitakatwa—katwa kiwe vitambaa, na walitaka kukiombea hapa usiku huu, pamoja na bahasha fulani zilizojaa. Nami nilidhani tungeweka hizi wakfu kwa—kwa Bwana. Hiki chote kitakatwa—katwa kisha vinitangulie kuenda Afrika. Sasa, mwajua vitambaa vingapi vitakavyokatwa kwacho vikiwa ukubwa huu, maelfu. Ndugu Fred alileta mia saba majuzi katika bahasha ndogo hivyo. Nanyi mwaweza kuwaza hiki—hiki kitakuwa vingapi. Kwa hivyo tuna... Kitambo kidogo tu, naam, tutaviombea.

² Sasa, nimepwewa sauti kidogo, lakini nilisema kuwa ingerudi kuyajibu baadhi ya maswali ha—haya vema niwezavyo. Na sasa, kila mara, wakati hii mikutano ya ufufuo ijapo, inaanzisha mchangamko mdogo. Nami nataka—niliwaza labda hili limesawazisha kanisa usiku huu, mwajua, kwa sababu wa—wakati fulani kitu fulani huenda kilisemwa ambacho kanisa halikufahamu. Nao walikupa nafasi kuandika swali lako mwenyewe sasa. Nitawapeni yale niliyo nayo; na ndiposa; kama mnayo mengine kama hayo, hayatawapasa kuyaandika.

Ndiposa moja wayo ni: **Tafadhali—eleza Warumi 7:25?**

Linalofuata: **Ulisema mtu anaweza kuishi karibu sana ma Mungu hata asitende dhambi.**

Tutakuwa na umbo gani katika ufufuo?

Ndugu Branham, Yambidi mtu afanyeje wakati wamekwisha fuata maagizo yote ambayo umefundisha; ndiposa, unampokeaje Roho Mtakatifu?

Tafadhali eleza Waebrania 6:4 na uilinganishe na Waebrania 10:26.

Na: Nini maana ya kuchaguliwa asili kabla kuwekwa misingi ya dunia, na ungepata hayo wapi katika Biblia?

³ Na Dada Mc... La, hi—hilo ni ombi la maombi.

⁴ Sasa, hayo ndiyo maswali yetu tuliyo nayo usiku huu. Kama una lingine tunapokuwa na utangulizi mdogo hapa, vema, lilete hapa, nasi tutajaribu tu... Sasa, kama kuna swali lolote mawazoni mwa kanisani kuhusu lo lote ambalo—tulilo nalo, naam, tungependa tu ku—kuweza ku—kuwasaidieni kadiri tujuavyo. Ona?

⁵ Nami nawatakeni ninyi kila wakati kukumbuka kuwa yale ninayosema hapa, sisemi ni Kweli bila shaka na kadhalika. Ni kadiri nijuavyo kuwa ni Kweli dhahiri. Ni—ningekosea kama tu mwanadamu ye yote, lakini mimi, Ndugu Jackson—najaribu tu kueleza katika njia ninayodhani sahihi (mwaona?), jinsi ninavyoiona, Ndugu Mike, katika Biblia, ku... Na kusoma kirefu mambo haya, siyachukui tu kutoka mahali pamoja. Ni—nitarudia na kuileta kutoka Mwanzo, na kuileta hadi Ufunuo, moja kwa moja kote katika Biblia.

⁶ Ndiposa, ungeleta ile—hata somo lile kote. Lakini, kama halilingani na mengineyo ndani mle, Maandiko mengineyo, basi ingekuwa si kweli haidhuru. Kama uliitoa mahali po pote, yabidi iwe—yabidi iingiane na Maandiko mengine yote. Mwaona? Na Maandiko yote yataingiana pamoja kama yamewekwa pamoja sahihi, kama... Ni kama tu mchezo mgumu wa fumbo. Nami simaanishi... Kama nimekosea, basi Mungu anisamehe. Maandiko ni kitu kama mchezo mgumu wa fumbo. Ona? Hilo... Yote yametengwa na kuchanganywa katika sanduku, na inahitajika Roho Mtakatifu kuyaweka hayo pamoja. Ona? Na—na hatuwezi kulifanya. Sasa, hakuna tafsiri 969 kwake, kwa sababu Biblia ilisema Maandiko si ya kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Ni kama vile tu yalivyoandikwa. Tunayaamini tu ku... (Asante, Ndugu Pat.) Sisi... Ni kama tu vile ime—imeandikwa katika Biblia; hivyo ndivyo itupasavyo kuyachukua, hivyo. Kwa hivyo tukijaribu kuyafanya yaseme kitu fulani hapa, vema, hayatakisema vivyo hivyo hapa basi, Ona, tuki—tukiweka... Yakubidi ufanye Maandiko yajijibu Yenyewe hapa, yajijibu Yenyewe hapa, Yajijibu Yenyewe hapa, kila moja yayo yaende tu mahali panapofaa kuyafanya yote yaingiane pamoja.

⁷ Na sasa, nilidhani labda... Nilikuwa nihubiri na nikasema ningehubiri usiku huu, *Tumeona Nyota Yake Mashariki, Nasi Tumekuja Kumwabudu*; lakini sina sauti ya kutosha, basi, kufanya hivyo. Nilikuwa nimepata joto hapa usiku mmoja hata nikatoka nje. Nami nilikuwa na joto sana nilipoingia garini, nilitokwa na mvuke. Nilifungua dirisha na kuenda nyumbani. Vema—nadhani hiyo ilikuwa Alhamisi au Ijumaa usiku. Usiku uliofuata, nikaanza ku—siku—nikaanza kupwewa sauti kidogo, kama ku... Ee, ni... Si—si kuwa mgonjwa, si homa, si ugonjwa, si mafua; lakini ni kama tu—kama ugonjwa wa kuumia kikoromeo kooni mwako kwa kuongea na—na kukiumiza kwa kuhubiri kwa nguvu, ndiposa—ndiposa ikafifia. Lakini ita—itapona baada ya siku moja au mbili, labda ifikapo Jumapili. Huenda nikaja kumsaidia Ndugu tena. Baada ya yeye kumaliza mahubiri yake, nitachunguza hapa na pale na kuona nini kingine kimesalia.

⁸ Ndiposa—ndiposa nataka kanisa lote limpokee Roho Mtakatifu. Sasa, binti mkwe wangu anaketi hapa. Si kwa

sababu yeye ni binti mkwe wangu, si kwa sababu yeye yuko hapa, yeye ni mmoja wa wasichana wazuri sana niwajuao; yeye ni msichana kipenzi, Loyce. Naye amepitia kwa vitu vikubwa toka utotoni mwake, ambapo ilimbidi yeye atoke kwa jamaa ambao hawakumwabudu Mungu na mengineyo. Namsikitikia mtoto huyu, ilimbidi akue hivyo. Na sasa yeye anamtafuta Roho Mtakatifu, na amefunga hadi ni vigumu kwake kusimama, akifunga na kuomba ampokee Roho Mtakatifu.

⁹ Dada yangu, Dolores, aliniambia, “Bill, mimi tu... Kanisa lilipokuwa—nguvu ilipokuwa kanisani,” yeye alisema, “nilijisikia tu kama ningepaa niende. Ndiposa wakati kila mtu—Roho Mtakatifu alipoanza kushuka juu ya watu,” kasema, “niliketi tu pale na kutazama hapa na pale.” Ona? Vema, ona, na swali hilo liko hapa usiku huu, juu ya hilo. Kwa hivyo niliwaiza labda hilo huenda likasaidia kanisani ku—kumpokea. Na sasa, sitaki kuchukua mkutano wa maombi wa Jumatano usiku na kuuvunja kwa kitu kama hicho, lakini ni—ninataka kuhakikisha kuwa kanisa laelewa mambo haya vilivyo (mwaona?), kabla...

¹⁰ Nami nilikuwa tu nikiongea na daktari fulani hapa Jumapili, akarudi nyuma ya kanisa hapa katika—nyuma hapa kanisani. Yeye alikuwa ni daktari wa madawa. Yeye alikuwa amekuja umbali huo wote toka (makao makuu ya Assemblies of God yako wapi sasa? Kule...) Springfield, Missouri, kuhudhuria mkutano.

Naye alisema, “Ndugu Branham...” (Sasa huyo atoka kwenye makao makuu ya Assemblies.) Na yeye alisema, “Maishani mwangu mwote nimeshangaa kuhusu hilo.” Kasema, “Ni mara yangu ya kwanza nimelifahamu maishani mwangu.” Yeye alisema...Alikutana nami nyuma kule chumbani, nimeketi, daktari wa madawa.

¹¹ Na—na kwa hivyo, Ndugu Mercer na Ndugu Gene Goad nyuma kule na vinasa sauti... Hivi sasa, Ndugu Mercer alisema alifaidika sana kwenye ule mkutano ambapo—ambapo tulieleza kuwa—kuwa Roho Mtakatifu alipoingia mkutanoni na—na kujigawanya Mwenyewe, na Mungu alijigawanya Mwenyewe kati ya watu Wake... Vema, hivyo tu ndivyo afanyavyo. Ndiposa, watu wa Mungu waanzapo kukusanyika pamoja, kuna umoja, kuna nguvu. Ona? Na wakati wo wote watu wa Mungu watakapoungana pamoja kabisa, naamini ufufuo atatokea wakati huo. Kutakuwako na wakati wa kunyakuliwa Roho Mtakatifu aanza kuwakusanya. Wao—itakuwa katika uchache, bila shaka, lakini kutakuwepo na kukutanika kukuu.

¹² Sasa, hizi nguo za kuombewa zinazotumwa, ile Sauti ya Uponyaji... Mimi mara moja, mwanzo wa mwaka, Bwana akipenda, Ni—ninaenda Kingston, Jamaica, hadi Haiti, na toka pale... Rais wa Haiti alinitumia mwaliko na—na majeshi yao yote kwa ulinzi. Wana maasi kule. Na jambo ni kwamba, yeye ataka tuje na aina hii ya huduma, ambayo alisikia ilikuwa

kule—kule San Juan mwaka uliopita yeye alipokuwa kule. Yeye alisema alidhani hicho ndicho kitu pekee ambacho kingeokoa nchi yake. Ona?

¹³ Sasa, iwapo nina rafiki Mkatoliki anayeketi hapa, sisemi hili kwa—kwa kuwaudhi ninyi wala cho chote kile; sikusudii hivyo. Lakini kanisa Katoliki linajaribu kuipindua serikali ya Haiti (ona?); na jambo pekee litakaloiokoa, ni ufufuo wa Kiprotestanti unaochochea hivi sasa. Ona? Na ulikuwa mzuri sana, nami naudhamini. Na kwa hivyo nilimwambia, wakati wa juma la Krismasi na siku chache zijazo sasa, baada ya kesho, tutaanza kufunga na kuomba, na kuona ni njia ipi Bwana atatuongoza.

¹⁴ Kisha Amerika ya Kusini . . . Ndiposa, najisikia nikiongozwa kuenda kule—kule Norway. Najisikia nikiongozwa dhahiri kuenda Norway mwaka huu, ndiposa, Afrika pia. Na hiki kina—kitakatwa katika vitambaa vidogo na kutumwa Afrika kabla ya mikutano ile. Hivyo ndivyo jinsi watu wengi . . . Mnaweza kupata wazo la vivi hivi jinsi watu wengi wanavyotumana nguo zilizoombewa sasa wanaposikia unakuja (ona?), wanaanza ku—kuwasiliana tena. Kwa hivyo hivi ni vitambaa vidogo vilivyokatwakatwa pia na tayari kutumwa kwa—kwa watu mbalimbali.

¹⁵ Kwa hivyo pamoja na hili Kanisa kuu la Mungu Aliye Hai, hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mchache sasa. Na kila mmoja wenu kwa njia yako mwenyewe, omba ili Mungu atie upako vitambaa hivi. Sasa, kwanza nanukuu Maandiko kuwa, “Toka kwa mwili wa Paulo walichukua vitambaa, au lesa, na kuviweka juu ya wagonjwa, na pepo wachafu waliwatoka watu, na mateso; nao waliponywa.”

¹⁶ Bwana, juu ya dawati hili ndogo ambalo limekuwa hapa kwa miaka hii yote, na jinsi Wewe umetubariki sisi sana, na I—Injili imepitia hapa, na . . . Kama dawati hili lingalikuwa na macho au lingenena, lingeeleza mamia ya miujiza mikuu ambayo imetendwa papa hapa mbele yake; viwete, vilema, vipofu, waliokumbwa na kansa. Na nguvu za Mungu Aishiye zimedhihirishwa katika jengo hili ndogo. Basi Baba Mungu, tunakushukuru tu Wewe kwa ajili ya mambo haya yote.

¹⁷ Na sasa, kanisa limekusanyika pamoja usiku huu kukuabudu Wewe. Tumekuwa kwa ajili ya—kujibu maswali ambayo yameulizwa. Ni unyofu wa mioyo ya watu ambapo mambo haya yanawatatanisha wao mawazoni mwao. Nasi Bwana, twatambua, kuwa kama jambo lo lote linatutatanisha, hatuwezi kamwe kuwa na imani, mradi tu kuna swali. Kwa hivyo hatutaki tuwe na maswali yo yote.

¹⁸ Bwana, twaona haja ya ubatizo wa Roho Mtakatifu kati ya watu wetu na kati ya kanisa hili. Nasi—nasi hatutaki kuwa na maswali yo yote niani mwao. Tunataka yote yajibiwe, kwamba

wao watajua ni nini Yeye ajapo, na kujua kwamba ni kwa ajili yao.

¹⁹ Ndiposa, katika nchi za ng'ambo, kule ng'ambo katika hizo pori zenye giza ambapo ngoma zinapigwa, na wenye ukoma wametapakaa kote kote—chini ya miti, na inzi zi—zikivuma, na ile—na miguu yao imekatika na masikio yao yameliwa na nyuso zao zimeliwa, na ukoma. Uvundo, Bwana, hadi ni vigumu kuwakaribia umbali wa jengo moja la mji. Na maskini, watoto wachanga bila chakula, bila nguo. . . Nao wananipenda, Bwana. Nao—wao wameamini huduma hii, baada ya zile Nguvu za Mungu Aishiye kuwaponya wengi wao. Nami sijapata raha rohani mwangu tangu nilipoondoka Afrika, nikijua kuwa maskini hao watu wa kusikitiwa wako katika hiyo hali mbaya pale, na wanaishi katika hali ushirikina. Na wale wachawi, wakiwa na mifupa ya wanadamu wakiigongagonga kwa vidole vyao, na kuita pepo, jamani, ni mahali namna—namna gani, ndiposa kuwaza, hapa Amerika, makanisa malidadi na mahali pakubwa. Basi, Mungu, na kujua maskini watu hawa wana mahitaji, kuwaona wao wakija mkutanoni, wamerundikana moja juu ya mwingine, na wengine wao wanakufa wakiwa wamelala pale, wakijaribu kusikia maneno machache toka kwa mtu fulani ambaye wamesema kuwa anakujua Wewe. Mioyo yao imeanza kuinuka, Bwana, kwa sababu Ujumbe na barua zinaenea kote Afrika sasa. Mioto, yaonekana, inaanza kuwaka tena.

²⁰ Na kanisa Lako kuu kule, ambalo lilikuwa kanisa kuu, lilivunjikavunjika, ee Mungu, na kimoja kikajitenga katika makundi ya kidehuri, na—na mengine yangali yanajaribu kushikilia ile Kweli na Roho. Na sasa, maelfu wanatumana sasa, wanataka vitambaa vya maombi upesi ambavyo ni—nimeviombea. Katika hizi bahasha ndogo hapa kuna mahitaji yetu ya maombi, ya vifurushi vidogo vinavyowaendea wanaohitaji. Ee, Mungu wa Mbinguni uliyeumba mbingu na nchi, nakuomba, Bwana, katika Jina la Yesu kuwa utatakas kila uzi wa hivi vitambaa. Na Roho Mtakatifu Wako aende na kila uzi wavyo, Bwana. Na vinapowekwa juu ya wagonjwa na wanaougua, na pepo wachafu wawaondokee.

²¹ Kuwaza kuwa nyuma kule katika hayo mapori ambapo vitu hivi vitaenda, ambapo wana—hata wanamwabudu shetani. Naomba, Mungu, kuwa yeye hatakuwa na mahali hata pamoja pa kusimama, ya kwamba yeye ataondoka kambini, na watu watapata kumfahamu Bwana Yesu. Tujalie, Bwana. Na magonjwa yao yaponywe, shida zao zitatuliwe, na nafsi zao zikokolewe, na Nguvu za Mungu zipate ushindi. Tujalie, Baba. Twatuma kila sehemu ya jora hii kama kitu kimoja. Ndimi nyingi za moto ziko humu usiku huu, Bwana, nasi pamoja twatuma maombi yetu Kwako kwa ajili ya hivi, kuwa kila mtu ataponywa vitakapowekwa juu yake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²² Sasa, mwaweza kunisikia nyuma kule, vizuri sana nyuma kule usiku huu sasa? Vema. Nadhani tutakuwa na furaha sana tutakapopata kanisa lingine hapa, kwa sababu vitu hivi vidogo vinafifisha, vinazuia sauti yako nanyi—nanyi ni vigumu kusikia kwa vyo vyote vile.

²³ Sasa, natambua tena usiku huu, nina—ninafikia mahali... Ndugu Wood, kabla sijasahau, nimekipata kitambaa kile. Je, si ulinipa kitambaa kwa ajili ya mtu fulani? Au haikuwa wewe? Mtu fulani alinipa kitambaa kukiweka mfukoni mwangu na kukivaa, na nimekuwa nacho tangu wakati huo, kwenye mkutano. Sijui ilikuwa nani. Nilidhani ni wewe uliyesema, “Weka hiki mfukoni mwako kwa ajili ya mtu fulani.” Baadhi... [Ndugu Neville amweleza Ndugu Branham kuhusu kitambaa kile—Mh.] Ndivyo ilivyokuwa? Ndugu Jackson, je, ulikuwa na kitambaa cha mtu fulani? Hiki hapa. Vema. Hiki... Vema, hiki kitakuwa papa hapa, Ndugu Jackson, ukitaka. Na sasa, najua mtu fulani alinipa, kasema, “Kivalie Mfukoni mwako.” Ndiposa, nilikiweka mfukoni mwangu na kukisahau.

²⁴ Sasa, ku... Sasa, Bwana akipenda, na sauti yangu imepona, ifikapo Jumapili asubuhi au Jumapili jioni, mojawapo, Bwana akipenda, nataka kuongea kuhusu ujumbe wa Krismasi nilio nao kwa ajili yenu. *Ile—ile Ishara Yakini.*, Mwaona? Mimi bado... Nimeupangia Jumapili asubuhi, ndiposa, kitu fulani kilichochea moyo wangu. Nami nilikuwa tu mbali sana na ujumbe kuurudia tena. Kwa hivyo ni—ninataka kuendelea nao Jumapili asubuhi, Bwana akipenda, au Jumapili usiku, mojawapo. Kwa hivyo mimi na Ndugu Neville tutapanga hayo.

²⁵ Sasa, kama vile Ndugu Neville amesema, nami pia nataka kushukuru kila mmoja wenu kwa ukumbusho wa Krismasi, kadi zenu. Ndugu na Dada Spencer, nilipata zenu. Na wengineo mbali mbali hapa walionitumia kadi zenu, kote, nazithamini pamoja na zawadi na kadhalika mlizonitumia. Bila shaka tunavithamini. Toka—toka kwa mke wangu, na mimi, na—sisi—na watoto, tunawashukuru. Tungalipenda kuwatumieni zawadi ya Krismasi kila mmoja wenu, lakini hilo hakika ni jambo gumu kwa mhubiri kufanya, sivyo? Vema labda walivyo wengi wa kutumiwa, singeweza kufanya hivyo. Mwaona? Ni... Lakini laiti ningaliweza kuwapa watoto, kila mmoja wao, kitu fulani. Hakika ningependa kufanya hivyo, lakini... Wahudumu hawawezi kufanya hilo. Ona? Kuna watu wengi sana kuenda kuwanunulia. Lakini sisi sote, nina hakika, mimi mwenyewe na wengine pia, kuwa tunayathamini kusanyiko letu. Mojawapo wa jambo kubwa zaidi ambalo nadhani mmefanya, ni upendo wenu na imani yenu isiyofifia ambayo mmeweka kwangu kama—kama mmoja wa wachungaji wenu hapa, na—mwaka huu.

²⁶ Ndugu Neville, hilo ni kwako pia, ndugu yangu mpendwa. Na roho mwema ambaye Ndugu Neville ameonyesha kila wakati, kama, “Njoo, Ndugu Branham; mimbara ndiyo hii,

hubiri. Mungu ahimidiwe, napenda kuketi na kusikiza.” Nami—napenda hilo. Na—napenda tu hiyo njia nyenyekevu, kunjufu aliyo nayo Ndugu Neville.

²⁷ Nanyi imani yenu yote, na... Jambo moja ambalo mwaweza kunifanyia kwa hisani, ni kuniombea. Sasa, nitafanya mikutano mbalimbali kadha kabla ule mpango mkubwa wa safari haujaanza. Sasa hiyo—hiyo itakuwa kule karibu Glasgow, Kentucky, nitahubiri usiku. Labda Campbellsville, Kentucky, nitahubiri usiku. Na—na pale mahali pengine kule Kentucky, Willow Shade, naamini ni huko, ninao usiku mmoja. Kwa... kuendelea tu hivyo, nitawaarifu mara tu baada ya kuinyosha, kuhusu mikutano inayokuja, ambayo itakuwa mahali mbali mbali sasa, hata nitakaporudia mikutano ya hadhara tena.

²⁸ Lakini nimejitolea mwenyewe upya na mara nyingine tena usiku uliopita kwa Mungu. Na kwa msaada wa Mungu na kwa neema ya Mungu nimeamua kushika hatamu mpaka nitakapokufa. Ona? nilifanya hilo yapata miaka thelathini iliyopita. Nami nimekuwa katika... Lakini ninachoka sana wakati mwingine, nikashindwa kabisa. Nafikia mahali ambapo siwezi kuendelea zaidi. Ona, ninyi ni vigumu kuiona papa hapa. Ninyi—ninyi hamjui kile kilicho juu pale, na ng’ambo kule, na humu. Na—na hata si kutoka kwa mmoja—si hata kutoka mji mmoja, la; jimbo moja, la; si kutoka Marekani; bali ulimwenguni (ona?), ulimwenguni kote. Ona? Na hao—hao ni wengi, nadhani, tunawasiliana usiku huu, nimekutana nao au kuwasiliana nao, si maelfu, bali mamilioni ya watu. Ona? Na utashangaa tu wangapi wa hao ni wagonjwa. Ona? Nao wanaita; na linaleta msongo mkubwa sana.

²⁹ Kwa hivyo nayathamini maombi yenu wote. Na kwa msaada wa Mungu na neema Zake, Krismasi Yenye furaha kwa kila mmoja wenu. Kumbuka msemu wangu, hii si Baba Krismasi hii ni ya Yesu. Mwaona? *Krismasi* maana yake ni “Kristo.” Nasi tulikuwa tukiendesha usiku uliopita tukiwaonyesha watoto nyumba zote zilizopambwa na kila kitu, ambazo ni malidadi sana. Lakini niliwaza, kama nikiwahi—cho chote nyumbani mwangu, nilichotaka kuandika, kingekuwa maandishi ya umeme: *Natumai Kristo Atakuwa Katika Krismasi Yenu*. Naam. Mrudishe Kristo katika Krismasi.

³⁰ Sasa, Baba Mungu, tunaendea maswali haya sasa. Tunayajia kwa unyofu sana. Na—na hawa watu wazuri, Bwana, wameyaweka maswali haya na—yaliyo mioyoni mwao, na labda wengine zaidi jengoni; nao wanataka kujua la kufanya. Na Baba, mi—mimi sifai kuwa mahali pako, lakini naomba kuwa utanisaidia kujua Neno Lako, kuwa nitaleta fungu la kutosheleza kwa kila swali. Hili basi twaliacha mikononi Mwako, na twaomba katika Jina Lako. Amina.

³¹ Sasa swali la Ndugu Pat hapa ni zuri sana, sana. Ama kweli nianzie kwalo, Ndugu Pat. Sasa, kama ye yote wenu mliosalia

ana swali, uliandike tu na uliweke juu hapa, au—au Ndugu Pat atakuletea karatasi kama huna karatasi; ama kweli nitafurahi kufanya kadiri niwezavyo kulijibu.

Sasa, hili ni swali hasa, Ndugu Pat. Hili laonekana kama la kuchekecha, lakini ni swali.

**101. Wako wapi wale pepo walioingia katika nguruwe wale?
Wako wapi wale pepo walioingia katika lile kundi la
nguruwe siku Yesu alipowatoa kutoka kwa yule mwenda
wazimu?**

³² Vema, Ndugu Pat, kwa kadiri ninavyofahamu...Sasa, tunaanzia kwanza kwa maarifa kuhusu pepo. Sasa, kufahamu pepo ni jambo kuu. (Sasa, wengine wenu chungeni saa na msiniache nichukue muda mwingi kwa swali moja.) Lakini hizo nguvu za pepo, hao pepo walikuwa katika mtu aliyeitwa Legioni kwanza. Sivyoy? Na sababu ya jina lake kuwa Legioni, ni kwamba *Legioni* katika Kiebrania maana yake ni “wengi.” Ona? Kulikuwa na wengi wao.

³³ Na pepo hao waliokuwa katika mtu huyo mpendwa walimfanya awe mwenda wazimu. Na iwapo mtu ye yote alipata kumwona mwenda wazimu au akamshughulikia, wana nguvu mara nyingi ku—ku—kupita kiasi, sababu wamepagawa sana na shetani. Kama umekuwa ambapo m—mtu alirukwa na akili, ee, inahitajika watu kadhaa wenye nguvu kumshika. Nao wana nguvu mara mbili au tatu ya nguvu zao.

³⁴ Sasa, mtu anapolemaa na Roho Mtakatifu amshike, ikiwa shetani ana nguvu nyingi kumfanya mtu awe na mara tatu au nne ya nguvu zake za kibinadamu, Mungu naye aweza kuweka nguvu kiasi gani katika mwanadamu? Ona? Hizo ndizo zimjiazio kumfanya atembeke katika nguvu za Mungu, ambapo yeye amekuwa mlemavu kwa miaka mingi. Mifupa yake inanyoka; na mikono yake inanyoka; yeye anatembea, kama kijana mwanamume mpya, kwa sababu nguvu za Roho Mtakatifu ziko juu yake.

³⁵ Sasa hawa walikuwa waovu sana hata walimfunga mtu yule minyororo, naye angeivunja. Nao walisema yeye aliivunja vipandevipande. Na hakukuwa na cho—cho chote ambacho angefungwa nacho. Bila shaka alikuwa katika hali mbaya, kwa sababu alikuwa na legioni ya pepo wengi ndani yake. Ndiposa, yeye alipo...Yesu alivuka na kuingia Gadara na kuanzia makaburini...Na yeye alikuwa mwovu sana, si mtu yule (ona?), mtu yule alikuwa sawa.

³⁶ Si mtu yule. Umwonapo mtu kama huyo, usithubutu kuwazia kuwa ni huyu mtu; ni shetani aliye ndani ya mtu yule.

Sasa, yule mwenda wazimu pale jukwaani usiku huo, angeniva, kule Oregon. Mtu huyo, nilipo—aliponijia, badala ya yeye kutema mate usoni mwangu na kuniita mimi “nyoka nyasini” mbele ya watu wapatao elfu kumi, vema, haikuwa huyu,

haikuwa mtu yule. Yeye ni mtu alaye, anywaye, alalaye, labda ana jamaa, na ana upendo, ni—ni kama tu nilivyo mimi au ulivyo wewe. Lakini ilikuwa shetani ndani yake aliyekuwa anafanya hilo. Ona?

³⁷ Basi huwezi kamwe kumfukuza shetani kwa nia mbaya. Yahitaji upendo kufanya hilo. Na upendo ni nguvu iliyo na uweza mkuu sana ulimwenguni. Sasa, ukitazama, shetani kila mara ni chuki. Chuki ni ya shetani. Na watu wamchukiapo mtu fulani, kumbuka, ni shetani mbaya wa kudharau au kuchukia. Haiwapasi kufanya hivyo.

³⁸ Mwakumbuka kuwa ile—ile . . . Yesu alisema katika mahubiri Yake kuwa mwombapo, “Baba yetu uliye Mbinguni,” . . . Naye akalifuatilia, akasema, “Usipomsamehe kila mtu kwa moyo wako makosa yake, wala Baba yako aliye mbinguni hatakusamehe wewe makosa yako.” Ona? Haikupasi kufanya hilo.

³⁹ Lakini sasa, shetani anapoanzisha nguvu za chuki (ona?) kukimbia jukwaani kuniva, ambapo yeye kimwili, yeye angeweza bila shaka, mara nyingi zaidi . . . Yeye angenishika, labda, kwa vidole vyake viwili, hapa mshipini hivyo, kwa sababu yeye alikuwa na uzani wa ratili 260 au 270; yeye alikuwa zaidi ya futi sita na nusu au futi saba, mtu mkubwa mno. Na . . . alimpiga mhubiri kwenye barabara za mji kwa ngumi yake, akamvunja mtulinga pamoja na utaya, na kumuumiza, akapeleka hospitalini. Yeye alichukia wahubiri. Ndiposa, alikimbia juu pale kuniva. Ona?

⁴⁰ Sasa, ndani ya mtu huyu kulikuwamo baadhi ya roho hawa waliotolewa kwenye nguruwe kule Gadara. Baadhi ya maskini watu hao wako hapa katika vituo vya wazimu, wakigongesha vichwa vyao kwenye pao za chuma, korokoroni. Kumbuka, mashetani hawafi kamwe. Mashetani ni hai daima, lakini kutakuwa na wakati ambapo mashetani hawana budi kufa. Wataharibiwa kabisa. Lakini sasa, wanaishi, nao wanafanya kazi kutoka kizazi hata kizazi juu ya wanadamu. Baadhi yao wako katika umbo la kansa; baadhi yao wamo katika umbo laa kifafa; baadhi yao katika umbo la kifua kikuu. Wanaingia katika mwili, lakini kwa nje, hawana nguvu mpaka wameingia katika mtu. Yawabidi kutenda kazi kupitia kwa mtu fulani, ambalo laleta wazo lingine, kwamba Roho Mtakatifu ni—anafunika dunia, lakini hana nguvu hata ameingia ndani yako na yangu.

⁴¹ Mungu ananitegemea mimi na wewe. Ona? Roho Mtakatifu . . . Dunia imejaa Roho wa Mungu, lakini amemiminwa. Lakini ha—hawezi kufanya kazi hata aingiapo ndani yetu, sisi wanadamu, afanye kazi.

⁴² Na shetani anataka kutuchukua kufanya kazi chini yake. Kwa hivyo asipokuwa na nguvu sana, yeye huanza kwa dhambi. Kama anaweza kuwaweka ndani ya mtu mwenye haki, mtu mzuri, na aendeleo tu na kujaribu kuwa mzuri hivyo; kama

yeye aweza kumshikilia hivyo hata atakapokufa hivyo tu ndivyo anavyotaka kufanya. Yeye amempata, kwa sababu haijalishi wewe u mwenye haki vipi, u mzuri vipi, u mwadilifu vipi, u msafi vipi, umwaminifu vipi, hutawahi kuingia Mbinguni hata umezaliwa mara ya pili. Yesu alisema hivyo. Kwa hivyo hakuna... Huyu... Hauna budi kuzaliwa mara ya pili, hauna budi kuzaliwa upya, au hakuna njia ulimwenguni kwako kuingia Mbinguni, au kuja kwa Kristo kamwe.

⁴³ Sasa, nilisema dakika chache zilizopita, ambalo laweza kuzusha mawazoni mwenu swali lingine, kwamba mimi—kwamba nimefundisha, na hilo ni kuhusu—kuhusu... Kwamba siamini kuwa kuna kuna kuzimu ya milele... Siamini Biblia inafundisha kuzimu kunakowaka moto milele na dawamu. Haifundishi, kwa sababu kama kuzimu ni ya milele na watu waendao kule wataadhibiwa milele, njia pekee ambayo wangedhibiwa milele, ingewabidi wawe na Uzima wa Milele. Na kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo uko katika Mungu. Ona? Kwa hivyo yabidi wafikie uangamizi (ona?); hiyo ni, miili yao inaangamizwa, ndiposa sehemu yao ya kiroho inaangamia. Hiyo ni kuteketea kabisa; hamna kitu tena. “Bila mzizi wala tawi.” Biblia inavyokuita. Wanaangamizwa kabisa.

⁴⁴ Pia naweza kuthibitisha kuna daraja Mbinguni, kuwa wao wote hawatakuwa sawa, lakini watakuwa na Uzima ule ule wa Milele. Lakini Biblia ilisema kwamba wafalme wa ulimwengu wataleta heshima yao na utukufu (Ufunuo 22)—watalete heshima yao na utukufu katika mji huo. Hilo lathibitisha kutakuwako na wafalme katika hiyo nchi mpya, wafalme na watawala. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake... Wao walisema, “Tutapata nini baada ya kuwaacha baba, na mama, na vyote kukufuata Wewe.”

⁴⁵ Yeye alisema, “Amin, nawaambieni, mtaketi juu ya viti kumi na viwili vya enzi, mkiyahukumu makabila kumi na mawili ya Israeli katika siku hiyo.” Ona, ni mwingine, ni utawala wa kidunia unaokuja utakao—utakaokuwa mkuu zaidi ya wote ule. Humo hakutakuwa na dhambi, hata hivyo watakuwa na watawala na kadhalika katika miji, wakati kila kitu kitaendelezwa katika njia ya Uzima wa Milele.

⁴⁶ Lakini waovu wataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao kulingana na matendo yaliyofanywa katika mwili, ndiposa wataangamizwa kabisa. Sasa, hebu kumbuka hilo. Ninyi mnaoandika kwa muhtasari, kumbukeni hilo.

⁴⁷ Basi jueni haya kutoka kwangu, kuwa kuna aina moja pekee ya Uzima wa Milele, nasi tunautafuta huo; na ni Mungu pekee aliye na Uzima wa Milele.

Hakuna Uzima wa Milele aina mbili, Uzima mmoja wa Milele, na huo pekee ndio udumuo. Na kumbuka, andikeni hili pia kwenye maandishi yenu: Kila kitu ambacho kimeumbwa,

kilicho na mwanzo, kina mwisho. Kila kitu kilicho na mwanzo kina mwisho, na ni kile kisichokuwa na mwanzo ndicho pekee ambacho hakina mwisho. Na kuna kitu kimoja pekee ambacho hakikuwa na mwanzo kamwe, na hicho kilikuwa Mungu. Na hiyo ndiyo njia pekee unayoweza kufufuka katika ufufuo, ni kuwa na huo Uzima wa Milele. Ona? Hivyo ndivyo tu utakavyowahi kurudi, ni kitu ambacho hakikuwa na mwanzo. Na unapompokea Roho Mtakatifu, ndani yako mnakaa Uzima ambao haukuanza kamwe na hauwezi kwisha kamwe; na mnapokuwa na Uzima huo ndani yenu, basi mna Uzima wa Milele na mu wana wa kiume na wa kike wa Mungu. Ona? Na huwezi kufa tena kama Mungu asivyoweza kufa, kwa sababu wewe ni sehemu ya Mungu.

⁴⁸ Tulikuwa na swali hapa muda mchache uliopita, ndani humu mahali fulani, linalohusu kuchaguliwa asili, linaturudisha kwenye jambo lile lile. Unakuwa sehemu ya Mungu, na kama Mungu alijigawanya Mwenyewe katika hiyo Nguzo kuu ya Moto, na hizo ndimi ndogo zikaenda juu ya kila mmoja wa watu wale, na ingali inafanya vivyo hivyo siku hizi. Tunaweza kuthibitisha hilo kwa ujuzi tulio nao, kwa mafundisho ya Biblia, kwa uchunguzi wa kisayansi, picha kuonyesha hiyo ndiyo Hiyo, kwamba Mungu hujigawanya Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. “Na kwa kuwa naishi, ninyi pia mtaishi,” Yesu alisema. Hatuwezi kufa. Hakuna kitu kama mauti kwa Mkristo; “Kwa kuwa yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, anaishi; na kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa (ona?)—kufa.”

⁴⁹ Neno *mauti* maana yake ni “kutengana.” Sasa, kwa kimwili, tunatengana kwa kutokuonekana kwa macho yetu, kwa sababu huo bado ni dhambi, lakini roho yetu ni ya Mungu ambayo haiwezi kamwe kutengwa na Mungu, kwa sababu sisi tu sehemu ya Mungu. Sisi tu—sisi tunaleta . . . Sisi tunarudishwa katika hilo wazo la Mungu. Kila kitu ambacho Mungu hufanya ni kikamilifu na cha milele. Na wakati mawazo ya Mungu yalipowazia ufalme wa watu ambao wangemwabudu Yeye, hayo mawazo ni ya milele. Ona? Hayawezi kuangamia. Kila Neno la Mungu ni la Milele. Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, mbingu na nchi pia zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita kamwe.” Ona? Ni ya milele pamoja na Mungu. Na “Mkikaa ndani Yangu na Neno langu ndani yenu. . .” Ona? Tunakuwa sehemu ya Neno Lake, sehemu ya Uzima Wake, kwa kuwa tu mwili wa mwili Wake, na mfupa wa mifupa Yake, na uzima wa Uzima Wake. Ndipo hatuwezi kuangamia tena kama Mungu asivyoweza kuangamia. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo.

⁵⁰ Mtu mdogo ameondoka hapa anayetoka Georgia, Ndugu Evans. Yeye amekua kote nchini. Na yeye ni msaidizi mkubwa wa rafiki yangu mwema, Oral Roberts; na yeye—yeye alisaidia mipango yake yote ya televisheni kote chini pale, na alifanya mambo mengine mengi. Lakini yeye aliniambia hivi juzi,

akasema, “Ndugu Branham, nilisomea shule ya Ndugu Jagger. Nilienda kila mahali; nilikaa nje kule kwa miezi mitatu. Nilikuwa nikiwinda; nilienda mahali mbalimbali, kila moja wapo, na haikufaa kitu. Singewahi kufikia mahali ambapo nilikuwa na yakini halisi (mwaona?) nikifanya *hili*, au nikifanya *hilo*, ama nifanyeje *hapa*, nifanye, nisiyafanye,” kasema, “hata niliposikia mafundisho yako.” Kasema, “Ndipo nikatosheka kabisa.” “Kwa maana mwabudu akiisha kusafishwa toka kwa dhambi zake asingejiona tena kuwa na dhambi.” Yeye amepita toka mautini akaingia Uzimani, na yeye ana Uzima wa Milele ndani yake unaokaa mle na hawezi kufa kama vile Mungu asivyoweza kufa. Ni Biblia hasa. Ona? Yeye amelindwa milele, kwa sababu ana Uzima wa Milele.

⁵¹ Sasa, hilo halimaanishi kuwa unaweza kutenda dhambi na kuendelea nazo, kwa kuwa utendapo dhambi unahukumiwa kwa ajili ya dhambi zako. Kweli hasa. Lakini mradi tu Uzima wa Milele umo mle, unaishi milele. Yesu alisema, “Yeye asikiaye Neno Langu (Yohana Mt. 5:24)—yeye ayasikiaye maneno Yangu, amwaminiye Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, na hataingia hukumuni, ame—bali amepita toka mautini kuingia Uzima.” Ona? Wote... “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza; na wote wanijiao mimi nita... Na wote anipao Baba watanijia Mimi.” Naam. “Wote anipao Baba watakuja kwangu.” Naam. “Wote anipao Yeye watakuja mwangu na hakuna ye yote wao atakayepotea. Nitawapa Uzima wa Milele na nitawafufua siku ya mwisho.” (Yohana Mt. 6) Ee, ni dhamana yenye baraka jinsi gani. Ona? Basi haikupasi kuogopa mauti na kushangaa.

⁵² Mungu ametupa hakikisho kamilifu kuwa sisi tu watoto Wake. Na kama watoto Wake, Yeye anaturudi kama ninavyowarudi watoto wangu, wewe unavyowarudi watoto wako. Wakikosea, tunawarudi. Watoto wangu waki—wakifanya kosa, basi ni wajibu wangu kama baba kuwarudi. Ndiposa, watoto wa Mungu wakikosea, ni wajibu Wake kama Baba, na Yeye atawarudini ninyi. Kumbuka tu hilo, utarudiwa. Lakini mradi tu u mtoto Wake, laiti ulimwengu usingekugusa, (naam!), kwa kuwa Yeye alisema, “Ingekufaa ufungiwe jiwe kubwa la kusagia shingoni mwako na kutoswa katika kilindi cha bahari kuliko kumkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio.” Naam. Hukumu hiyo utakuwaje!

⁵³ Sasa, Ndugu Pat, tunarudia swali lako. Pepo wale waliotoka kwa mtu yule, wale waliomfanya mwenda wazimu (ona?), wanafanya vivyo hivyo siku hizi ndani ya watu. Ona? Ni pepo hao maelfu mara maelfu. Na shetani huingia tu na kitu kama kasumba kidogo. Ni kama tu wanapomchukua maskini msichana mwanafunzi; jambo la kwanza watakalofanya ni kumfanya avute sigara. Ona? Hilo humwamsha. Na watakayofanya baadaye, watapata nguvu zaidi kidogo.

Hatimaye, muda si muda, inaishia kwa bangi; halafu baadaye, atakuwa na tabia halisi ya kutumia madawa ya kulevyia. Inafanyaje? Inawafanya wenda wazimu. Wanakuwa na kichaa, na shetani amewapata. Ona?

⁵⁴ Kwa hivyo shetani yuko katika kuvuta sigara. Hiyo ndiyo hali yake ya chini. Sasa akikuona u mwerevu na utaona hilo, yeye hatakuacha uendelee zaidi ya kuvuta sigara. Ona? Kwa kadiri awazavyo tu kukushikilia wewe pale muda mrefu kutosha, amekatiza maisha yako, kwa sababu yeye ajua kuwa huwezi kuondoka mpaka Mungu amesema hivyo. Lakini utasikia mahubiri baada ya mahubiri, ujumbe baada ya ujumbe ukitiliwa mkazo baada ya mkazo, na onyo baada ya onyo; na kama tu angalikuepushia hayo na kuweka mawazo yako kwa kitu kingine, kama kuwa mtu anayeheshimiwa, au yakubidi uwe nayo, au kitu kama hicho, basi atakushikilia tu pale hata atakapokuondolea mbali. Au akiweza kukufanya tu ujiunge na kanisa na kusema, “Nitakuwa muungwana. Nitafungua ukurasa mpya. Nitapata . . . nitaenda kule kanisani na kujiunga na kanisa.” Yeye akiweza tu kukuweka chini ya hilo, hilo tu ndilo awezalo kufanya. Yeye bado amekushikilia wewe, kwa sababu wewe . . . Yesu alisema, “Amin, Amin, (hilo ni hakika, hakika), nawaambieni, mtu asipozaliwa mara ya pili kwa maji na kwa Roho, yeye hataingia katika huo Ufalme.”

Hebu nikuonyeshe tu kitu fulani. Nilikuwa naongea na ndugu asubuhi hii, Ndugu Wood, tulipokuwa safarini, nje kule, kujaribu kutuliza mawazo yangu, kujizuia nisingee ili nirudiwe na sauti ya kutosha kuhubiri usiku huu.

⁵⁵ Sasa, tazama! Tunaenda humu na kupata punje kubwa nzuri ya mahindi. Ni hindi kamilifu sana lililoko nchini. Sasa, ninaenda . . . ? . . . hindi au suke, vyo vyote mnavyoiita. Nita—nitalipeleka juu hapa kwa maonyesho ya Wilaya ya Clark, nami nitashinda zawadi kubwa. Ni punje bora ya hindi, hindi kamili sana lililoko, nililowahi kuona. Nitapata zawadi kubwa kwake. Nitalipeleka chini kwa ya Wilaya ya Floyd; nitalipeleka kwa Wilaya ya Harrison, nitaiipeleka jimboni, nami nitalipeleka kwa ya taifa. Na kushinda kila tunzo. Ni punje kamili kabisa la hindi. Na wanasayansi na darubini zao kuu, watazame ndani yalo, na kulifanyia uchunguzi. Ona? Lile . . . Lina shura kamili ya kutosha, na madini ya chokaa kamili, na—na uchepe kamili. Kila kitu kiendacho katika punje hiyo ya hindi ni kamili hasa. Sasa unasema, “Nitapanda hilo nipate punje nyingine kamilifu kutoka kwayo.” Na unaipanda hiyo ardhini. Isipokuwa hindi hilo, hiyo mbegu halisi, iwe na chembechembe ya uzima ndani yake, itakaa pale na kuoza, na huo ndio mwisho wake. Haitachipuka tena, haijalishi ni kamili vipi. Hai—haitachipuka isipokuwa na uhai mpya wa asili ndani yake.

⁵⁶ Na unaweza kumchukua mtu . . . Sasa, sikusudii hili kuumiza dhamiri zenu, nina . . . Hili ni kanisa, haya ni maskani

yangu, nami niko huru kama ndege. Ona? Sasa nawatakeni mkumbuke, kuwa katika hili, kuwa mtu anaweza kuwa mzuri; yeye anaweza kulipa fungu lake la kumi, yeye anaweza kuwa mwaminifu; anaweza kuwasaidia wajane; anaweza kuwasaidia yatima; anaweza kuwa mshiriki wa kanisa. Huwezi kupata hitilafu moja kuhusu mtu huyo. Kila wakati jambo fulani linapotokea, anaingiza mkono mfukoni mwake, atoe senti ya mwisho aliyokuwa nayo kuwapa maskini. Yeye ata—yeye atakusaidia kwa heri na kwa shari. Atakuwa mwenzi msiri wako wakati hata wale wengine wanaojiita hivyo watakukataa na kadhalika; na mtu yule bado ako nje ya Ufalme wa Mungu isipokuwa amejazwa na Roho Mtakatifu, Uzima wa Milele. Naam! Hivyo ndivyo ilivyo muhimu.

⁵⁷ Hiyo ndiyo sababu najaribu kufanya kanisa langu lifahamu hivyo. Nami—naomba kuwa usijaribu kufikiri tu eti najaribu kujifanya mwerevu kulihusu. Ni—ninajaribu kuwaambia ninyi kuwa shetani ni mdanganyifu sana, kwamba yeye bado anadanganya hata ye—yeye atakufanya utende kama Mkristo. Yeye atafanya kitu fulani kuiga Kristo hata kwa aliye Mteule. Biblia ilisema wangepanana sana. Utakuwa mtu mzuri. Utakuwa na . . .

⁵⁸ Sasa tazama hapa, hebu nikuonyeshe mifano usiwe na tashwishi sasa. Tunataka kuliweka katika Maandiko hali tukiwa kwa roho hizi. Esau alikuwa mtu mzuri zaidi kwa kila hai kuliko Yakobo alivyokuwa. Sasa, Esau (Mungu anisamehe kwa matamshi haya), yeye alikuwa tu maskini mwenda kifichifichi. Hivyo tu. Sasa, ukimtazama, yeye alikuwa nani? Mpayukaji na mwongo mkuu. Sasa, kama—kama nimekosea, Mungu anisamehe, lakini yeye alidanganya. Na kusema uongo, ilikuwa vigumu kumpata mmoja kama yeye. Yeye alipochukua hivyo vijiti vyenye milia na kuviweka majini kuwafanya wale ng'ombe na kondoo wenye mimba pale wazae kondoo wenye milia na ng'ombe wenye milia, kuwafanya wa—wake . . . Yeye alifanyaje? Alivaa koti la Esau na kipande cha ngozi ya kondoo na vinginevyo, na kuenda kule na kumuiga Esau mbele ya babake kipofu aliyekuwa nabii. Sivyo? Naam, yeye alikuwa maskini mwenye hila, ndivyo hakika. Na Esau alikuwa . . . Haingenipasa—labda haingenipasa kusema hivyo. Ona? Sikusudii hivyo. Ni—nitaomba radhi kwa hayo. Yeye—yeye alikuwa—alikuwa . . . Sijui, mwajua yeye alivyokuwa. Ona? Wazeni tu niani mwenu; nita . . . Yeye alikuwa—alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu, na sitaki kusema lo lote baya kumhusu (mwaona?), lakini najaribu tu kuonyesha jambo ndo—ndogo ambalo yeye alifanya. Mwaona jinsi alivyokuwa mwenda kifichifichi. Mwongo? Hakika, yeye alikuwa tu—alikuwa mbaya sana. Lakini alikuwa anajaribu kufanya nini?

⁵⁹ Mtazame Esau. Esau alikuwa mtu mzuri, mwadilifu, mshiriki wa kanisa mzuri leo. Alifanyaje? Alikuwa mwindaji.

Yeye alitoka nje...Bila shaka wakati huo, hivyo ndivyo walivyopata riziki zao. Yeye angeichunga mifugo ya baba yake. Baba yake alikuwa kipofu. Nabii, nabii wa Bwana alikuwa kipofu na akadanganywa na mwanawe binafsi, nabii, Isaka; kupitia kwake akaja Kristo. Mnaweza kumwita nabii, Biblia ilisema yeye alikuwa vile. Na alikuwa kipofu? Mbona hakujiponya mwenyewe? Mbona basi asijue kwamba huyo alikuwa Esau—kwamba huyo alikuwa Yakobo badala ya Esau? Ona? Mungu hawaambii manabii Wake kila kitu. Yeye huwaambia tu vile Yeye anavyotaka wajue. Ona?

⁶⁰ Mungu alikuwa akitengeneza mpango wakati huo, naye ilimbidi aufuata. Mungu... Ukijitolea mwenyewe kwa Mungu, Mungu atakufanya utende kazi moja kwa moja katika mpango Wake.

⁶¹ Sasa, tazama yale aliyosema, yale mtu huyo alifanya. Esau alijitahidi kumshughulikia maskini babake mzee na kipofu; na Yakobo, yaonekana, yeye hakumjali. Lakini kulikuwa na kitu kimoja Yakobo alichotaka, na hicho kilikuwa haki ya mzaliwa wa kwanza. Haidhuru itakuwaje, ataipataje, atafanya nini, yeye alijali tu ile haki ya mzaliwa wa kwanza. Na Esau, Biblia ilisema, alidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza; Biblia ilisema hivyo. Na Biblia ilisema, “Wasije washerati ovyo kati yenu, kama huyu mtu mwovu Esau aliyedharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza na kuiuza kwa ajili ya chakula kimoja...”

⁶² Sasa, haki ya mzaliwa wa kwanza ni nini? Ni ile haki. Hilo ndilo ninalojaribu kuwaambia ninyi sasa. Huyu Roho Mtakatifu ndiye Haki yako ya Mzaliwa wa Kwanza; huyo ndiye Haki yako ya Mzaliwa wa Kwanza. Hiyo ni haki yako uliyopewa na Mungu. Sasa, watu wangesema siku hizi, “Nitakwenda kanisani. Mimi ni mzuri tu kama jirani yangu. Lakini mimi, kutenda kama hao watakatifu wanaojigaragaza? Si mimi.” Vema, ewe Esau! Ona? Ni jambo lile lile, kudharau ile haki ya mzaliwa wa kwanza. Naam, yeye aliibadilisha kwa chakula cha dengi. Nanyi mnaiuza... Sasa, sisemi ninyi, lakini ulimwengu unaiuza kwa mambo machache zaidi.

⁶³ Esau alikuwa na njaa. Lakini, mwaona, kama wema ungehesabiwa... Kama mtu fulani... Kama tungetembea kule na kukaa pale hemani kwa siku cha—chache, tungetambua kuwa Esau alikuwa... Tungemchagua Esau. Ona? Lakini ndani ya moyo wake yeye alitaka hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza. Yeye hakujali kingine cho chote; yeye alitaka hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza. Hicho tu ndicho alichotaka.

⁶⁴ Na Esau alitaka kuwa mtu mzuri, na kushughulikia kila kitu, na kufanya kila kitu sawa tu, na kufanya kila kitu tu kama... Yeye alikuwa mfuata sheria kwa dhiti; Esau alikuwa vile, Yeye alitaka kila kitu sawa. Na Yakobo alitaka jambo moja, na hilo lilikuwa ile haki ya mzaliwa wa kwanza, na hilo tu ndilo alilolijali. Na Esau... Mwaona kilichotendeka kwa wavulana

hao wawili. Ona? Na hata toka kwa Yakobo kulitokea wale wazee wetu kumi na wawili waliozaa, vema, yale makabila kumi na mawili ya Israeli, kutoka kwa Yakobo. Naye alimwita— na Mungu alimwita Yakobo mwanawe. Mwaona ninalomaanisha?

⁶⁵ Huyo Roho Mtakatifu yabidi awe muhimu zaidi kwako kuliko kingine cho chote kilichoko ulimwenguni, sifa zako, maisha yako, kazi zako, kila ulicho nacho. Yakubidi usikome mpaka umempokea. Huna budi kumpokea. Sharti liwe jambo kuu zaidi. . . Nawe unasema, “Vema, naogopa kule—hiyo kazi yangu. Naogopa kwamba mume wangu, wangu. . .” Usiogope; acha Huyo achukue nafasi ya kwanza. Achilia mengine yote. Hebu Huyo awe wa kwanza. “Vema, natarajia kumpokea hivi karibuni, Ndugu Branham.” Si hivi karibuni, sasa! Huu ndio wakati. “Hebu awe wa kwanza mimi—kabla sijafanya lingine lo lote. Hebu nimpokee sasa!” Kukata tamaa! Hilo lingesaidia kujibu swali letu. Unapata—unapokata tamaa kwa ajili Yake, kweli huna budi kumpokea au ufe (ona?), wakati huo ndio utakapompokea.

⁶⁶ Maskini Myahudi mmoja aliishi hapa mjini. Sijui kama mnamjua au la. Yeye aliponywa ugonjwa wa kansa. Wakatoa—wakamfukuza. Naye alipobatzwa kwa Jina la Yesu Kristo, ndipo walimfukuza kabisa, wakamfukuza uwanjani. Ndiposa akaenda na kujiunga na kanisa la Methodisti. Nao walipotambua kuwa yeye alikuwa amebatzwa kwa Jina la Yesu, walimpeleka nje kwenye hali ya anga ya kipimo cha sufuri, yapata kumi chini, kule Ohio; wakamweka kitandani nje kule (Ndugu Freeman, bila shaka anamkumbuka Ndugu Vance, sivyo?)—wakamweka nje—nje kule, na mfereji wa maji nje pale, na kusema, “Kuna maji ya kutosha kwako kubatizwa kwa Jina la Yesu, nadhani.”

⁶⁷ Walakini, yeye alikuwa akinisimulia hadithi ndogo wakati mmoja. Alisema wakati watu *fulani*, mke wake—walikuwa wanakaa na. . . Na yeye alikuwa amekusanya vitu vyake vyote vikuukuu kwenye gari kuukuu lililovunjika na kuondoka mjini. Na mke wake akasema, “Wajuaje? Laiti ningalikunywa maji kabla sijaondoka huko.” Kasema, “Nasikia kiu.”

Vema, akasema, “Mpenzi, kuna bomba la maji.”

Kasema, “Vema, endelea hadi ufike mahali pazuri zaidi.” Mwaona?

Naye akaenda mbele kidogo, na kusema, “Bomba la maji lingine ndilo lile.”

Kasema, “Vema, endelea.” Mwaona?

⁶⁸ Lakini kasema, “Kisha, mwanamke yule alipoingia mashambani, hakukuwa na bomba la maji.” Kasema, “Yeye alikuwa tu akipigania maji ya ku—kunywa.” Naye kasema, “Baada ya muda mchache, kule mbali mashambani kulikuwa na bomba kuukuu la mashambani, kule mbali mashambani,

kote kupitia kwa kundi la ng'ombe; naye alikuwa anaogopa ng'ombe." Lakini yeye alisema, "Mwanake yule kasema, 'Levi, sharti ninywe maji!'" Kwa hivyo wao—yeye akasimamisha gari. Na kusema, kabla hata hajasimamisha gari kabisa, yeye alikuwa nje akitimua mbio kuelekea bomani. Ilimbidi apate maji. Na Mungu awapo halisi hivyo kwako, basi unapoonna kiu hivyo, ya kwamba au eti ni Mungu au utakufa, huwezi kujizuia tena, ndipo jambo fulani litatendeka. Yabidi—unakuwa na shughuli na Mungu. Huo ndio wakati unapochukua—linapotendeka.

⁶⁹ Sasa, hawa roho wabaya huwadanganya watu. Na roho hao, wakati mwingi ni wa kidini mno. Sasa unasema, "Unamaanisha, wa kidini?" Naam, bwana: Hata wanafundisha Maandiko, Biblia. Bila shaka hufanya hivyo.

⁷⁰ Sasa tazama! Yesu aliwajia kundi la watu waliokuwa makuhani watakatifu; nao walitii sheria vilivyo; nao walikuwa wa kidini mno. Na Yesu—Yohana aliwaita wao, kasema, "Enyi wazao wa nyoka (yaani wao majoka), ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja?" Yesu alipowaona, Yeye alisema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi." Huyu ni Mungu aliyesema hayo. Wa kidini tu kama walivyoweza kuwa.

⁷¹ Kumbuka, wakati—shetani humchukua mtu wake, bali si roho yake kamwe. Mungu humchukua mtu Wake lakini si Roho Wake. Ona? Roho Mtakatifu anaingia maishani mwako na kutakasa roho yako, anaishi kupitia kwako, na kukupa wewe nguvu za kuishi. Lakini wakati—wakati roho yako inapoondoka, roho yako inalindwa na Mungu; lakini Roho Mtakatifu aliyekuwa juu yako anakuja juu ya mtu mwingine, na mtu mwingine, na mtu . . .

⁷² Roho huyu aliyekuwa juu ya Eliya alikuja juu ya Elisha, sehemu Yake maradufu; miaka mia saba baadaye au miaka mia nane baadaye akaja juu ya Yohana Mbatizaji, akamfanya yeye atende . . . Tazama jinsi Eliya, tazama jinsi Eliya alivyokuwa: mtu mkubwa mwenye nywele nyingi, mwingi wa sharafa; ngozi ya kondoo, alionekana kama mdudu mwenye manyoya, uso wake nje hivyo, akichapa miguu pale, mwenye ngozi kiunoni, mshipi wake kama—mshipi kiunoni, hivi. Kama ungekuwa na . . . Kama yeye angetembea hadi nyumbani kwako ungesema, "Mama wee! Iteni polisi upesi sana. Mtu wa kutisha amesimama mbele ya mlango wangu." Lakini huyo alikuwa nabii wa Bwana. Hakika: Ndiposa, yeye alipokufa, sehemu maradufu ya Roho wake ilimjia Eliya; kisha miaka mia nane baadaye akamjia Yohana Mbaptizai na kumfanya Yohana atende tu vivyo hivyo kama wao walivyotenda, kwa sababu ilikuwa roho wa Eliya.

⁷³ Sasa, kama roho wa Eliya juu ya Yohana angemfanya Yohana atende kama Eliya, Roho wa Mungu juu yako atakufanya utende kama Yesu. Sasa, hapo ndipo unapompata Roho Mtakatifu. Ona? Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu atendavyo. Anakufanya mpole, anakufanya mnyenyekevu, anakufanya wa kusamehe.

⁷⁴ Je, wangeng'oa sharafa usoni mwako, kama ungekuwa nao pale, kuzing'oa na kutema mate usoni mwako, hali ulikuwa na nguvu kuita je—majeshi ya Malaika? Ungefanya hivyo kwa ajili ya upendo wa watu waliokuwa wakikutemea mate usoni mwako? Je, ungefanya hivyo? Kama mtu fulani angekuja hadi ulipo na kusema, “Hee, wewe mnafiki!” na kukupiga kofi shavuni, je ungewaombea msamaha? Sasa, hapo ndipo tumaini—jaribio kama una Roho Mtakatifu au la. Ona? Wakati mtu fulani asemapo maovu dhidi ya mtu mwingine, wakati mwingine anayedai ana Roho Mtakatifu, “Atanijuta hata inichukue hata siku ya mwisho.” Ona? Sasa, hapo ndipo unapochunguza Roho Mtakatifu wako. Ona? “Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanena kila neno baya kwa uongo kwa ajili ya Jina Langu.” Lakini unaenda na kujilipizia kizazi? La: “Furahini, na kushangilia, kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.” Ona?

⁷⁵ Mtu fulani asemapo neno baya kukuhusu, neno jambo zuri. Kama huwezi kusema jambo nzuri kumhusu, basi usiseme lo lote. Sahau. Ona? Ndiposa, unapojirudia, waombe.

⁷⁶ Kama kuna jambo moja maishani mwangu lililonisaidia kufahamu kuwa Roho Mtakatifu alikuja ndani yangu pale siku hiyo, limekuwa hilo. Nilikuwa mwenye hasira, mkali, M-Irishi pande zote mbili. Nami kila mara ilikuwa vigumu kula, mdomo wangu kila mara ulikuwa umepondwa-pondwa ambapo mtu fulani aliuponda-ponda, nikirukia ambapo singepaswa kurukia. Baadhi ya meno yangu yamevunjika sasa na kujazwa ambapo ni—nilinena ambapo haingenipasa kunena (mwaona?) na kusema mambo . . . Kila mara katika shida. Nami nilisema . . . Mtu fulani aliniambia, mwalimu wangu shuleni, yeye alisema . . . Nilisema, “Bibi, si—si—siwezi kujizuia.” Ona, ningeingia shidani wakati wote. Nami nilisema, “Siwezi kujizuia.” Maskini mkongwe Mama Temple, alienda tu Utukufuni majuzi.

Naye alisema, “Vema, tazama hapa Mpendwa.” Alinipakata miguuni pake, naye akanikumbatia kwa mikono yake akaanza kulia. Ndiyo mara ya kwanza kupendwa na mtu ye yote hivyo, mwanamke mkongwe. Yeye alililia tu juu yangu. Naye kasema, “Billy, nitakufanyia kitu fulani, Mpendwa; nitakupa uzi mdogo.” Na kasema, “Ye yote wa vijana hawa akikurukia . . .”

⁷⁷ Waliniita “mtafuna-mahindi,” kwa sababu nilitoka Kentucky, mwajua, na—na . . . Nilikuwa nikivalia vibovu mno. Nao walifanyia mzaha nywele zangu, zikining'inia karibu refu kama zilivyo sasa, na chini kuufunika uso wangu. Nami nilikuwa na wakati mgumu, mwajua. Na—na wangenipiga kila mahali na kunipiga makofi. Wakati wo wote ye yote alipokasirika, wangekuja, na kunishika, na kunipiga makofi. Na hapa ninge kuja. Ona? Na—kwa hivyo basi—na mapigano. Nasi tuli—tuliwapa wao . . . Hata nilishiriki mapigano ya visu na kadhalika.

⁷⁸ Nilichukua bunduki muundo wa Winchester na kujaribu kuwapiga risasi, na kuwaelekezea wavulana wanne au watano, kwa kunipiga hata ikawa vigumu kwangu kusimama. Ningeua kila mmoja wao kama tu haingekuwa Mungu. Niliyachukua maganda toka ardhini, na kuyarudisha ndani ya bunduki ile; ilikuwa ikifyatuka tu kama ilivyowahi kufanya. Ona? Ningalikuwa muuaji wa wanaume watano, labda, au wavulana watano.

⁷⁹ Nilikuwa tu na umri wa miaka ipatayo kumi na miwili, mwenye hasira kali! Na mwalimu alisema, “Chukua huu uzi mwebamba, Billy, na unaposhikwa na hasira sana, unatulia tu na kufunga vifundo tisa katika uzi huo.” Kasema, “Ufanyapo hilo, ndipo uniletee uzi huo. Nakuhakikishia hasira yako itakwisha.”

⁸⁰ Nilisema, “Bi. Whalen, nadhani u mzuri sana.” Nilisema, “Ni—nitajaribu hilo.” Ona? (Au Bi. Temple; nilisema Bi. Whalen. Nilisema Bi. . . .Bw. Whalen alikuwa mwalimu hapa wakati mmoja.) Kwa hivyo nili—niliweka uzi ule mfukoni mwangu. Nami sikuwa bustanini kwa dakika tano hata mtu fulani aliponipiga moja. Vema, nilianza—niliufikia, mwajua. Niilingiza na kunyakua uzi wangu; nikaanza kufunga kifundo kimoja; nikautupa chini, nikaondoka. Ona? Singeweza kulifanya. Ona?

⁸¹ Nami nilisema, “Singeweza kamwe kuwa Mkristo.” Lakini hebu niwaambieni, usiku huo kule kwenye Barabara ya Ohio, Roho Mtakatifu alipoingia ndani yangu, huyo alituliza hasira ile. Hiyo ilikuwa imekwisha. Nilisema, “Singeweza kamwe kulifanya. Singeweza kamwe kuwa Mkristo, kwa sababu singeweza kuishinda hiyo,” nilisema, “kitu nilichoza liwa nacho.” Nilisema, “Wee, baba yangu alikuwa na hasira kali; na—na mama yangu, nusu Mhindi, hasira ya kutosha kupigana na msumeno.” Nilisema, “Mimi? Ee, ni. . . .Wee, mtu ye yote anayenirukia ataona; hivyo tu.” Nilisema, “Kama itanibidi nipande ngazi ili niwapige,” nilisema, “hakika nitafanya hivyo.” Ona?

⁸² Lakini sasa, unaweza kunivuta nje pale na kunivurumisha chini na. . . .Ona? Mbona? Si mimi! Ninajaribu kusema nini hapa? Kitu fulani kilitendeka. Hiyo nguvu ya kale, huyo William Branham wa kale alikufa, na mtu Mwingine akaingia. Na lanifanya niwasikitikie maadui wangu. Mtu fulani anifanyiapo lo lote baya, siombi dhidi yao, nawaombea. Na hapo ndipo Roho Mtakatifu aliponijaribu usiku mwingine kule New England, kabla hili halijatendeka hapa. Wakati hilo—wakati Yeye alipotoa mamlaka, kasema, “Nena tu utakalo kwa watu hawa.” Jinsi walivyofanya. . . .Nami nikatazama pale, na nikasema, “Nawasamehe ninyi.” Hivyo ndivyo alivyotaka hasa. Ona? Wasameheni adui zenu. Ona? Hao ndio pepo wanaokufanya wewe mwovu. Chunguza pepo hao.

⁸³ Hapa kukatokea mtu fulani. Yeye alikuwa juu kule kaburini. Mtu fulani alikuja, yeye alikimbia na kuwashinda, Biblia ilisema. Hakuna ye yote—yeye alikuwa hatari sana hata hakuna mtu angepitia njia hiyo. Lakini siku moja kulikuwako na Nguvu kuu zaidi iliopita. Yeye alikuwa amepagawa na chuki, wivu, pepo, majeshi yao yakitembea pale, mtu mkubwa. Wangeenda nje pale, na kuchukua jeshi, na kumfunga minyororo; naye angeivunjavunja hiyo minyororo. Na shetani alikuwa ndani yake. Ndiye huyo. Yeye ange...?...Yeye angekuwa—yeye angekuwa kipenzi hasa wa Shule ya Sekondari ya Jeffersonville. Hakika! Ndiye huyo, baadhi ya...Au baadhi ya hawa matineja, mwajua, “Ee yeye ni mwanamume hasa.” Nimemwona mtu aliyekuwa na uzito wa ratili mia mbili wala hakuwa na wakia moja ya mwanamume ndani yao. Huyo si mwanamume, huyo ni mnyama. Ona?

⁸⁴ Lakini kulikuwa na mtu mdogo, aliyejikunyata mabega aliyetembea barabarani siku moja, aliyejikunyata (Biblia ilisema hakukuwa na uzuri hata tumtamani Yeye, mwenye umri wa miaka thelathini na anaonekana kama aliyezidi miaka hamsini), akitembea barabarani siku moja. Naye akakimbia kule kukutana naye. Kasema, “Nitamshika tu huyo mtu mdogo na kumwangamiza.” Lakini, jamani, yeye alipokutana na Huyo, alianguka miguuni pake. Pepo hao walimpagaa sana...Sasa tazama. Siku hiyo...Yeye alipagawa sana na pepo... .

⁸⁵ Sasa hili, nataka kuweka hili ndani—kwa ajili yenu. Yeye alikuwa—huyo alikuwa amejitolea kabisa kwa pepo, hata shetani alitumia ulimi wake kunena. Sasa, unaweza kujitolea sana kwa Mungu hata Mungu aweza kuutumia ulimi wako. Hiyo ni kweli! Hilo ndilo ninalodai. Mahubiri yo yote niliyowahi kuyahubiri yaliyokuwa na maana yo yote kwayo, ni wakati nilipojitolea, nilipomwondoa William Branham njiani na Kristo angeingia na kuanza kuongea. Ona? Na Yeye aweza kunena kwa lugha.

⁸⁶ Sasa tazama. Yeye alipagawa sana na huyo pepo mchafu, na pepo huyo alimshika sana hata...Hao pepo walijua wakati wao ulikuwa umewadia, kwa sababu walikutana na upendo.Ona? Nao walisema, “Tutamjaribu.” Na wote...Sasa, tazama yale yaliyotendeka. Yeye alisema, “Naam, sisi tunajua wewe u nani. Mbona wewe uko katika mwili mdogo kama huu, huyu mtu mwembamba?” Kasema, “Mbona umekuja hivyo?” Kasema, “Tunajua wewe u nani. Wewe u mtakatifu wa Israeli, basi mbona una...?” (Sasa tazama! Kama huamini kwamba kuna mateso yajayo ya pepo, sikia hawa wakikiri) “Mbona umekuja kututesa kabla ya muhula wetu?” Walijua kulikuwa na mateso yanayokuja. “Mbona umekuja kututesa kabla ya muhula wetu?” Ona?

Kisha Yesu akasema, “Jina lako ni nani?” Yeye alijua; Yeye aliwataka wakiri.

Kasema, “Sisi tunaitwa Legioni, kwa kuwa tu wengi.” Yeyealisema, “Ukitutoa kwa mtu huyu. . .”

⁸⁷ Tazama, mtu mwembamba kama Yesu amesimama pale (ona?), na mtu ambaye angepiga karibu jeshi nzima; hata minyororo haingemzuia. Ona, si nguvu za kimwili. Hilo silo jambo muhimu. Jambo muhimu ni ile nguvu ya Roho Mtakatifu iliyo ndani ya maisha yako. Ona?

⁸⁸ Yeye alisema, “Usitutese kabla ya muhula wetu; lakini ukitutoa. . . (Tazama uchoyo wao, uovu ule.) Ukitutoa, usituache tuzurure tu bure ulimwenguni, kwa kuwa ni vigumu kujua kama tutamwingia mtu mwingine. Ukitutoa. . . Tunataka tuwe ndani ya mtu fulani; tunataka kufanya kitu fulani; tunataka kutenda ubahili mwingine.” Huyu ni shetani. “Atanijuta,” [Ndugu Branham aonyesha sura ya uchoyo—Mh.] Ona? Huyu ni shetani. “Atanijuta.” Ona? Kumbuka tu, ni ndugu yako anayesimama pale, lakini shetani amempata. Ona? “Hebu tutende ubahili. Tunaweza kuwafanya hawa Wagerasi hapa wajutie hili,” labda walisema ku. . . Kiongozi wao alisema, “Turuhusu twende chini kule katika lile kundi la nguruwe.”

⁸⁹ Yesu alisema, “Nendeni. Lakini tokeni ndani yake!” Ee, lo! Mtu mdogo kama huyo akinena na kundi hilo kubwa la pepo. “Tokeni kwake! Nendeni.” Nao waliingia katika nguruwe hao, nao wakashikwa na kifafa, ikawafanya nguruwe hao kuwa na kifafa. Basi wakateremka mbio moja kwa moja hata mtoni, na kuzamia majini, wakafa maji mtoni. Sivyo?

⁹⁰ Sasa, wakati walipofanya hivyo. . . Bila shaka pepo wale waliwatoka kwa sababu waliwaua hao nguruwe. Waliwafanya wawe na hasira ya ghafula. Walipatwa na hasira ya ghafula kama mtu ye yote. Je, umewahi kumwona mtu ameshikwa na hasira ya ghafula? Vema, hivyo tu—hivyo ndivyo ilivyo. Hao ni pepo. Hayo ndiyo yaliyotendeka kwao. Ukiwahi kumwona mmoja wao akiwa na hasira ya ghafula, useme, “Enhee, najua yale yaliyotendeka kule Gerasi sasa.” Ona? Hiyo ni kweli hasa. Wengine zaidi waliingia ndani mle, wakamfanya wazimu kabisa; bila shaka daktari wa madawa atakwambia hasira ni hatua ya kwanza ya uenda wazimu. Hivyo ndivyo Mayo wasemavyo, hatua ya kwanza ya uenda wazimu.

⁹¹ Ndugu Pat, hilo huenda limekuwa jeuri. Hilo ndilo bora nijualo, bila kutarajiwa tu. Vema.

102. Warumi sura ya 7, kifungu cha 25.

⁹² Yanibidi ku. . . nilisahau, nilisoma hayo hivi majuzi nilipokipata, lakini nasahau chasema nini. Hebu na tujibu swali la huyu mtu mpendwa tukiweza. Warumi 7:22, vema. Ishirini na tano, samahani. Warumi 7. . . nilifungua kurasa mbili mara moja. Ona?

*Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu.
Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili—kwa—*

kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.

Sasa ngoja kidogo. Sikukisoma barabara.

Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu... (Naam, ndivyo)... naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.

⁹³ Vema. Hivyo ndivyo hasa Paulo alivyosema mara nyingi. Nifanyapo mema, maovu yako. Ona? Hivyo ndivyo ufanyavyo pia. *Kwa akili zako*, huo ni moyo wako. Ona? Sasa kumbuka, huwazii kwa nia yako; wala huoni kwa macho yako. Wala hu—hufanyi—hufanyi... Unaona kwa moyo wako. Ulijuua hilo? Je, ulijua moyo wako ulikuwa na mtu mwingine ndani yake mbali na wewe? Sayansi iligundua hayo yapata miaka minne iliyopita, mwajua. Chumba kidogo moyoni, wanamosema nafsi huishi.

⁹⁴ Je, mliwahi kusikia kuhusu dhamiri? Unaanza kufanya kitu cho chote, na unawaza, “Ee, nitakimalizia tu kileleni,” lakini dhamiri yako inakwambia tofauti.

⁹⁵ Wanaweza kuchukua chombo cha kugundulia uongo... Namwona rafiki yangu, Attorney Robinson, ameketi nyuma kule. Nami sijui kama mmewahi kuona ikifanywa au la, lakini nimewahi kuwekwa—kupelelezwa—kiliwekwa kwangu wakati mmoja, kuhusu huyu Malaika wa Bwana hapa. Nao wanakiweka kile chombo cha kugundulia uongo kwako, na unajaribu katika—kukiri kadiri ujuavyo, vizuri uwezavyo kuyanena, vizuri tu na kulainisha yote, kwamba hukufanya *jambo hilo*—mvunja sheria. Hicho chombo cha kugundulia uongo kitageuka na kusema unadanganya. Ona? Mbona? Mtetemo wa neva zako ndio wanaopekua kwa hicho chombo cha kugundulia uongo. Ona? Ki—kitakwambia. Kwa sababu gani? Mwanadamu hakuumbwa adanganye kwa hali yake ya asili. Ni dhambi na shetani aliye juu yako ndiye anayekufanya udanganye. Ona?

⁹⁶ Hu—hukuumbwa upate kudanganya. Hiyo ndiyo sababu yakubidi uishi tena, kwa sababu uliumbwa, uliumbwa uishi milele, kuishi daima. Lakini ona, dhambi iliingia na kuletea mwili mauti. Ndiposa, dhambi iingiapo na kuletea mwili mauti, basi bila shaka mwili huna budi kufa. Lakini ni—ndani mle mnaweza kudumu Uzima wa Milele, wakati roho hii imegeuzwa ndani yako na una Uzima wa Milele. Mungu ataufufua mwili huo tena siku ya mwisho. Yeye alisema Yeye angefanya hivyo.

⁹⁷ Kwa hivyo kwa akili—mawazo... Yeye alisema katika mahali pengine, “Nadhani nina nia ya Kristo.” Sasa, katika nia hiyo unatumikia—kwa nia ya Kristo unamtumikia Mungu. Ona, sehemu ya ndani (ona?), ile sehemu ya ndani, unamtumikia Mungu. Hiyo dhamiri ya ndani hapo ndipo imani ya ndani hukaa.

⁹⁸ Nataka kuwaulizeni. Kulikuwako wakati wo wote ambao ninyi watu ndani humu, wengi wenu mmeona wakati ambapo mnge—mngejua tu kitu fulani kingetendeka. Ilionekana kama hakingetendeka, lakini ulijua, ulijua kitatendeka. Je, uliwahi kuwa na hilo? Hiyo ni ile imani, hiyo dhamiri iikitenda kazi.

Sasa, kama kunakuwa na joto ndani humu, mnaweza kufungua chombo hicho kule chini, kama inakuwa na joto sana kwenu.

⁹⁹ Sasa, ndani mle hiyo dhamiri (ona?), hapo ndipo nia yako . . . Sasa Yesu alisema, “Mtu asipozaliwa mara ya pili . . .” (Sasa, hilo silo nililotaka.) “Amin, Amin, nawaambieni, mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi *kuuona* Ufalme wa Mungu.” Sasa, hungeona Ufalme wa Mungu, kwa sababu Ufalme wa Mungu ni Roho Mtakatifu. “Wapo katika hawa wanaosimama hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata wauone kwanza Ufalme ule ukija katika nguvu,” Yeye alisema. Kisha, “Ufalme wa Mungu,” Biblia ilisema, “umo ndani yenu.” Umo ndani yenu, Roho Mtakatifu, nawe huwezi kuona huo kwa macho yako. Kwa hivyo *kuona* maana yake ni “kufahamu.”

¹⁰⁰ Umewahi kutazama kitu cho chote, ukakikodolea macho, kasema, “Vema, sikioni.” Ona? “Sikioni.” Unamaanisha hukifahamu. Ona, Ona? Hukifahamu. *Kuona* ni “kufahamu.” Lakini kwa macho yako wewe hutazama kitu cho chote, lakini kwa yale yaliyo ndani yako, unafahamu kwayo, mwaona hilo. Ona? Unatazama kwa macho ya Mungu.

¹⁰¹ Na sasa, shikilia jambo hilo muhimu sasa. Hapa kuna zuri kama mko tayari: Mkristo hutazama vitu ambavyo yeye haoni kwa macho yake (ona?), kwa maana tunatazama vile visivyoonekana. Ona? Unavitazamaje? Kwa jicho lililo ndani. Unaiona kwa imani. Na sasa, kuthibitisha hilo: silaha zote za Kikristo zimeundwa kwa vitu visivyoonekana. Silaha za Kikristo ni nini? Mtu fulani asema, “Kuona ni kuamini.” Mtu huyo hangeweza kamwe kuwa Mkristo, kwa sababu silaha za Mungu zimeundwa kwa huu: upendo. Je, umepata kuuona? Umeuona katika matendo, lakini hujawahi kuuona upendo. Huwezi. Chomoza sehemu yako ya upendo nione sura yake. Ona? Upendo, upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, imani—imani, utu wema (ona?); silaha zote za Kikristo hazionekani kwa macho ya kawaida, lakini zinafahamika kwa moyo! Naam. Basi.

¹⁰² Paulo alisema, “Kwa akili zangu . . . (‘Nami nina nia ya Kristo . . . ? . . .’ alisema.) Namtumikia Mungu kwa akili zangu, lakini kwa mwili wangu (yeye alinenaje pale hatimaye?)—lakini kwa mwili, sheria ya dhambi.” Ni nini? Mwili wangu wasema usiku huu, “Umechoka sana. Koo lako limekauka sana. Una—umekuwa nje kwenye upepo leo. Hutaenda kanisani usiku huu.” Hiyo ni sheria ya mwili. “Heri umwite na kumwambia Ndugu

Neville kuwa... Peleka maswali kule na acha yeye ayajibu.” Lakini mwaona, niliahidi kutenda hayo. Ona?

¹⁰³ Sasa, akili zangu, kule ndani Roho Mtakatifu alisema, “Tekeleza ahadi yako.”

Lakini mwili ulisema, “Umechoka sana.” Ona?

¹⁰⁴ Sasa, mwili unasema, “Sasa, hakuna haja, wewe mtu mdogo mrembo, ndiwe mrembo sana shuleni. Sasa, usimsikize kamwe yule mama yako mtakatifu anayejigaragaza au huyo baba yako mshupavu wa dini. Ona? Wewe ndiwe msichana mrembo sana shuleni.” “Wewe ndiye mvulana wa kupendeza sana, mvulana anayeonekana bora zaidi, mwenye maungo bora sana. Wewe u maarufu sana mjini.” Mwaona? Hilo—hilo... Na ukitoa viungo vyako kwa hayo, basi utatokea wapi? Hatarini kila wakati. Ona?

¹⁰⁵ Paulo alisema, “Mwili wangu unataka—unataka kila mara kujitolea kwa hilo.” Mwili wako unafanya hivyo pia. Ona? Lakini sheria ya Roho wa Mungu moyoni hushinda mwili na kufanya mwili utii yale moyo unayouambia ufanye. Haleluya!

¹⁰⁶ Tazama, basi kama itafanya hivyo kwa mwenye dhambi, je, si itafaa kwa ajili ya magonjwa pia? Sheria ya Roho wa Mungu moyoni inayojua kwamba “Kwa kupigwa Kwake tuliponywa,” zinasimama kwa nguvu zao zenyewe kufanya ugonjwa huo katika mwili huo uzitii, kwa sababu ni shetani. Naam. Whiu! Hilo lina siagi nyingi hivi. Nawaambieni. Ndivyo. Ona?

¹⁰⁷ Sasa, sheria ya dhambi na mauti inafanya kazi katika mwili wako, lakini sheria ya Roho wa Uzima inafanya kazi moyoni mwako. Kwa hivyo moyo wako, roho yako iliyo moyoni mwako itaufanya mwili wako utii vile usemavyo ufanye. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, hayo ndiyo Paulo aliyosema. Kila wakati mwili, “Nimechoka sana; nimeshindwa; sistahili; siwezi.”

Ni—nilimwambia Loyce hapa, au Dolores, au mtu fulani aliyekuwa akiongea nami kuhusu Roho Mtakatifu, kuhusu kitu fulani, nilisema—nikisema, “Nini...”

Dolores akasema, “Nini—nini kilinifanya nijisikie hivyo wakati ambao ilinipasa kujisikia vizuri?”

¹⁰⁸ Nikasema, “Shetani. Yeye alikuona tu uko tayari kuupokea. Akasema, ‘Nitamlowesha kidogo [Ndugu Branham afanya sauti kuonyesha—Mh.], kumpulizia hewa kidogo, mwajua, kumpoesha kidogo.’ Ona? Lakini jamani; hapo ndipo unapoinuka! Dai haki zako ulizopewa na Mungu.” Hilo ndilo Paulo alilokuwa akimaanisha. Ona? Ile... “Kila mara wakati—” yeye alisema, “Nifanyapo mema, maovu yako.”

¹⁰⁹ Nitakwambieni la kufanya. Nimetambua hili, mimi na mke wangu... Nami nitajaribu kuharakisha, kwa sababu nina dakika chache tu zaidi, nami nina maswali makubwa hapa. Sitaki kuwakawisha sana, lakini nataka kupata maswali yenu vizuri niwezavyo.

¹¹⁰ Tazama! Naweza kuanza asubuhi, na kusema ninaenda... Sasa, Bwana ananiongoza kuenda mahali fulani kwa ajili ya mkutano, vema, ndugu, utazame tu kila kitu kikitendeka. Au uache nifike nyumbani kwangu, na simu toka mbali ziingie. Sasa, yanibidi niombee wagonjwa. Maskini Joseph atapanda shingoni mwangu. Sara atataka kuniuliza swali. Becky ataanza kupiga kinanda. Nasema, “Shii, shii, shii!” Nikiwapungia mkono, “Heei, shii, shii, shii, shii, shii, ninaenda ku—baba anaenda kuombea wagonjwa.”

“Vema, baba, tazama; Joe alifanya hiki...” Mwaona? Hebu ianze tu. Na mara tu ombi linapokwisha, wanachukua wanasere na kuwa watulivu na wazuri sana. Ni shetani. Hakika ndiye.

¹¹¹ Ndioposa nitarudi na kusema, “Joseph, usifanye kitu *fulani*.” Nawe wajua, muda si muda, yeye amezoea. Na utayapata katika watoto, watakudanganya. Vema, huyo ni roho wa udanganyifu juu ya mtoto huyo. Kuna tiba moja tu kwalo. Siwazii mdeki wa bunduki, sio wazo langu, mwajua, mdeki tuliokuwa tukipigiwa nao, Ndugu Jess. Tulipopatwa—tulipopatwa—tulipopatwa na shida tulikuwa tukiondoa mdeki kwa zile bunduki zilizozeeka, kile kijiti cha jozi, mwajua, bunduki ya fataki ya zamani. Siwazii hayo. Lakini kuomba, mtote shetani katika mtoto huyo. Naam. Maombi hutenda hayo.

¹¹² Kama maskini Molly anaanza kukwaa miguu yake midogo, na kuenda nje, na kuinua mapua yake madogo juu, ungempiga mpaka asiwe na nguo yo yote; yeye angefanya hivyo haidhuru. Lakini nenda tu mbele za Mungu ukadai nafsi ya mtoto huyo kwa Mungu. Endelea kusihi. Naamini ndilo jambo bora sana nilijualo. Naam, bwana: Hiyo ndiyo dawa bora sana nijua, ni maombi.

103. Sasa, hebu tuone. Sasa linalofuata hapa lasema, **Nini maana ya kuchaguliwa tangu awali kabla ulimwengu haujaanza; kuko wapi katika Biblia?** Kuchaguliwa tangu awali kabla ulimwengu haujaanza?

¹¹³ Vema, rafiki yangu mpendwa, hebu tufungue Waefeso sura ya 1 mahali pamoja tu. Hatutakawia kwa hili sidhani, isipokuwa lisijibike sahihi. Basi hebu tuanze kusoma hapa katika Waefeso sura ya 1.

¹¹⁴ Sasa jambo la kwanza, nataka kusema hili, kwamba *kuchaguliwa tangu awali* ni neno baya kwa muhudumu ku—kutumia mbele ya makutano ambayo hayaajafundishwa. Ona? Ndivyo. Silitumii. Wakati mwingine hapa kanisani... Lakini nje kwenye makutano, nje kunako... Ambapo—kila kitu kimerundikana toka kwa kila kitu, natazama neno hilo. Mimi kila mara hutumia neno kujua tangu zamani, kwa sababu *kuchagua tangu awali* ni kujua tangu zamani tu kwa Mungu. Mungu akiwa asiye na mwisho, kwa kujua tangu zamani Yeye

alijua kila kitu, au Yeye si asiye na mwisho. Ona, ona? Yeye alijua yale yangetendeka. Kwa hivyo kwa kujua tangu zamani Yeye angechagua tangu awali. Hiyo ndiyo sababu naamini kwangu Mungu—kwamba Mungu hafanyi tu . . .

¹¹⁵ Kama tu hewa mnayopumua: sikubaliani na Mashahidi wa Yehova kwa wazo kwamba pumzi yako ndiyo roho yako. Haiwezi kuwa. Ona? Roho yako iko moyoni mwako. Ona? Nawe ulikuwa na roho yako kabla huja—hujapata kuja ulimwenguni. Mungu alimwambia Yeremia kwamba Yeye alimjua, akamtakasa na akamfanya nabii kwa na mataifa kabla hajakuwepo tumboni mwa mamake (ona?), Yeremia 1:4.

¹¹⁶ Sasa tazama. Kwa hivyo twaona kuwa mambo haya yote ni kujua tangu zamani. Miaka mia saba na kumi na miwili kabla Yesu hajazaliwa—kabla Yohana hajazaliwa. Isaya alimwona katika ono, kasema yeye alikuwa sauti ya mtu aliaye nyikani—miaka 712. Tangu bustanini mwa Edeni, Yesu Kristo, kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu . . .

¹¹⁷ Ilikuwa je . . . ? Hebu tusome hili. Waefeso 1, hebu tuanze sura ya kwanza ili—samahani, kifungu cha 1.

Paulo, mtume . . . (Sasa tazama jinsi yeye anavyotangulia hapa. Napenda njia hii ya Paulo. Napenda Paulo, nanyi je? Ee, yeye alikuwa mtumishi wa ajabu wa Kristo. Sasa tazama haya.)

Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu; kwa watakatifu walioko Efeso, na . . . wanaomwamini Kristo Yesu.

¹¹⁸ Tazama, haya hayakuandikiwa ulimwengu; haya hayakuandikiwa walio nje. Haya ni kwa Kanisa lililo katika Yesu Kristo (jamani, si hilo ni zuri?), Kanisa lililoko katika Yesu Kristo. Hilo ni . . . Unaingiaje katika Yesu Kristo sasa? Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili mmoja. Sasa vipi . . . Na—naye anaelekezea hiki watu waliojazwa na Roho Mtakatifu (ona?), si ulimwengu wa nje.

Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.

Atukuzwe Mungu, Mungu Baba wetu—Mungu na—Baba wetu wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za ulimwengu wa roho—na baraka za rohoni katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo;

¹¹⁹ Jamani! Si ungependa kukaa katika baadhi ya huo? Vema, tumo humo. Hakika! Roho Mtakatifu yule yule. Kasema sasa, kama mnavyoketi pamoja katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo Yesu, Mungu ametubariki kwa baraka zote za rohoni, Dada Rose. Naamini—kwamba—hilo ni . . . Singe—singekumbuka jina lako hivi majuzi. Naamini ulikuwa katika mstari wa wanaohitaji maombi au kitu fulani. Nami—nikijaribu

kulikumbuka baadaye, nami—lakini jina lako ni Rose Austin, sivyo?...?...Ulikuwa ukija hapa maskanini kila mara. Naam. Vema. Sasa:

Atukuzwe—Mungu, Baba wa...Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohani—rohoni—katika ulimwengu wa roho...(Hebu tuone kama ninasema hilo—ninanukuu hilo sahihi.)

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohani, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo Yesu; (Tumekutanika pamoja sasa katika ulimwengu wa roho katika Krito Yesu.)

Kama...(sasa sikia; Je, nyote mko tayari?)... Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla...(sijawahubirieni ninyi). kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu,...

¹²⁰ Sasa, ona, yeye aweza kuzungumzia Kanisa. Yeye hangewaambia hayo watoto, lakini yeye anaongea na Kanisa ambalo tayari liko katika Kristo. Sasa, yeye hangeenda nje hapa kwa kanisa moja na aseme, “Vema, sasa...”—hilo. Ni Wale waliochaguliwa walio katika Kristo.

¹²¹ Sasa, wasema, “Vema, naamini kwamba mimi niko katika Kristo.” Kama uko, umempokea Roho Mtakatifu, kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee unaweza kuingia katika Kristo. I Wakorintho 12:13 (ona?)—I Wakorintho sura ya 12. Vema. “Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa Mwili mmoja (ambao ni ule Mwili wa Kristo).” Sasa! Ndipo tunaketi pamoja katika ulimwengu wa roho katika nia moja, Roho Mtakatifu akitenda kazi yetu, akitufundisha, akituonyesha sisi mambo makuu, akiyafanya yatimie. Lo ni mahali pa jinsi gani.

¹²² Yeye alisema, “Sasa, ninyi ambao mmeitwa hivyo, nataka kuongea nanyi, mlio wateule. Ambao Mungu alituchagua katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wazia hilo. Mungu alituchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu alijua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu kwamba ningehubiri somo hili usiku huu. Yeye hana mwisho. Na kabla kuwepo ulimwengu...Ee: Whiu! Po—pokea Roho Mtakatifu sasa. Neno litamleta. Ona? Hivyo ndivyo Yeye ajavyo: “Petro alipokuwa akisema maneno haya Roho Mtakatifu akawashukia.”

¹²³ Kabla ulimwengu haujakuwepo wewe ulikuwa katika nia ya Mungu kukupa Roho Mtakatifu, kwa sababu Yeye alijua kuwa utamhitaji; na Yeye Mwenyewe alikuchagua wewe kwa sababu ulitaka... Yeye alikuchagua wewe katika Kristo kabla wewe au Yesu, ye yote wenu, kuwepo duniani. Na Yeye alimtuma Yesu afe, akaandae njia ya kumtuma Roho Mtakatifu, kukuleta Kwake.

Ee, hilo tu ni... Ninajua huenda nika... Hili ni kanisa, kwa hivyo niko nyumbani sasa. Jamani, hilo ni zuri sana kwangu mimi. Kuwaza si lile nililotaka; si kutaka kwangu; si mapenzi yangu; si kuchagua kwangu; sikuhusika hata kidogo. Lakini kabla ulimwengu haujaanza, Mungu alituaona na kuweka majina yetu kwenye kile Kitabu cha Mwana-Kondoo cha Uzima. Kabla hata ulimwengu haujakuwepo! Nena kuhusu Mungu! Whiu!

¹²⁴ Nilisimama ng'ambo kule ambapo hiyo darubini kubwa... unaweza kuona miaka milioni mia na ishirini ya upeo wa nuru angani. Nilipotazama na kuona kwamba (mimi sikuona kwa kioo, lakini niliona picha ambapo walipigia)—nami ilinibidi kuinua mikono yangu ndani mle, mahali pale, nami nilisema, "Jinsi Wewe ulivyo mkuu, jinsi Wewe ulivyo mkuu!" Na kabla mojawapo wa hizo sayari haijazunguka (Haleluya!); Mungu alituchagua sisi katika Yesu Kristo. Sasa, jinsi Wewe ulivyo Mkuu. Naam, bwana!

¹²⁵ Kabla ulimwengu haujakuwepo, kabla sayari haijakuwepo, kabla jua halijakuwepo, kabla kuwepo mwezi, kabla kuwepo nuru, kabla kuwepo lo lote, wakati ilipokuwa bado ni Mungu, Mungu na mawazo Yake, lile wazo la milele la Mungu lilikuchagua wewe kwa kuchaguliwa tangu zamani, kwa kujua tangu asili kuwa wewe ungekuwapo duniani, kujua kungekuwapo dhambi.

¹²⁶ Mtu fulani alisema, "Basi, kwa nini—mbona kukawa na dhambi?" Kama hakungekuwepo dhambi kamwe, sifa Zake hazingalikuwa Mwokozi. Ilibidi kuwepo mwenye dhambi ili Yeye apate kuwa Mwokozi. Ilibidi kuwepo mgonjwa ili Yeye awe Mponya. Amina! Naam. Ilibidi iwe hivyo. Mungu ndiye ambaye—ambaye aliliona na kuchagua hilo tangu asili. Shetani hata hayuko mbioni. Ee, yeye ni chombo tu kandoni mwa njia ambacho Mungu alikitumia kuwaleta watoto Wake kwake, wakilia, "Aba, Baba." Si ajabu siku hiyo Malaika wataimba! Tutakapokuwa tukiimba nyimbo za hadithi za ukombozi, Malaika watainamisha vichwa vyao; hawajui yale tunayoongea. Hakika! Wao hawakupotea kamwe. Hawajui ni nini. Hawajui jinsi tujisikiavyo vizuri, kujua kuwa sisi ambao kwa wakati moja tulikuwa wenye dhambi na wageni kwa Mungu, pasipo tumaini, pasipo neema, pasipo Mungu katika ulimwengu wa uharibifu, vifo, tukielekea kuzimuni mwa shetani; Naye Mungu akainama chini, akatuchukua, na kutukomboza; na sasa sisi ni wakuu kuliko Malaika. Hivi sasa!

¹²⁷ Ni nini? Malaika ni mtumishi. Sisi tu wana wa kiume na wa kike. Nani anayewaziwa sana, mtumishi wako au mwanao au bintiyo? Jamani! Maombi ya mtakatifu yataenda mara milioni juu zaidi ya Malaika (naam, bwana!), kwa sababu yeye ni mwana. Naam hiyo ni kweli ndugu yangu, dada.

¹²⁸ Hu... Kanisa... Siamini upande huu wa... wa milele jinsi tutakavyotambua jinsi wewe ulivyo, mahali ulipo, ambapo

Mungu amekuweka, ninyi watu mliojazwa Roho. Ninyi mu wana wa Mungu. Naam, Malaika ni watumishi. Wewe u mwana! Malaika aweza tu kuleta ujumbe, lakini yakubidi utende. Amina! Wewe ndiwe mtendaji jukwaani. Wewe u mwana. Malaika ni watumishi kukuletea wewe ujumbe. Kasema hapa, “Nimekuletea wewe ujumbe huu ufanye *hiki na kile*. Hii ni kutoka kwa Baba. Nakuletea wewe. Naam!” Hivyo tu ndivyo ilivyo. Amina! Ninyi ni wana wa kiume na kike wa Mungu. Alituchagua tangu asili; Sasa, tazama tu kwa dakika moja.

Kama vile alivyotuchagua—alivyotuchagua... (Sasa, hatukuchagua...Ningemchagua Yeye vipi? Miaka bilioni, milioni bilioni, triloni mia nne iliyopita, ningemchagua Yeye vipi? Lakini Yeye alinichagua. Amina! Eee, Ndugu Wood, ndivyo. Ona?)...alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu. (Sasa, usijaribu kuifanya wewe mwenyewe, kwa sababu huwezi.)...watu—wasio na hatia mbele zake katika pendo.

Ee, ndugu, hilo litajibu swali nililoona ndani humu dakika chache zilizopita. Mahali fulani ni—nililiona tu...Ee, naam. Mlisema, “Mtu angeweza kuishi juu ya hili... (Kukatizwa kwa ukanda—Mh.]... angekuwa bila dhambi.” Sikiza hili:

...watakatifu...kabla ya kuwewa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo:

¹²⁹ Upendo wake ulitenda hayo. Upendo Wake ulilipia dhambi zangu. Upendo Wake uliziondoa. Upendo ndio nguvu kuu zaidi zilizopo. Mchukue mume anayempenda mke wake kabisa, yeye angejitolea kufa kwa ajili yake. Na upendano wa kindugu...

¹³⁰ Kulikuwako mtu, mtu fulani, aliyekuja kanisani humu mara kwa mara, toka barani. Alikuwa ameketi nyumbani mwa ndugu yake hivi majuzi. Yeye alisema, “Vipi kama kitu fulani kingetendeka kwa Ndugu Bill?” Yeye alisema, “Kwa furaha ningetokeza kifua changu nipigwe risasi kwa ajili yake.” Ona? Kukufia wewe. Huo ni upendo. Hakuna upendo ulio mkuu alio nao mwanadamu kuliko wao watakaotoa maisha yao kwa ajili ya ndugu ya—yake. Ona?

¹³¹ Katika upendo, ametuchagua katika upendo kabla ulimwengu kuwekwa misingi. Sasa tazama:

Kwa kuwa alitangulia kutuchagua...(Sasa, pale kuna neno kutuchagua)...Kwa kuwa aiitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na—sawasawa na uradhi wa mapenzi yake.

¹³² Na hilo je, Ndugu Mike? Si hilo ni la ajabu? Yeye alikupenda. Yeye alikupenda wewe kabla ulimwengu haujakuwepo. Yeye

alijua tabia yako; Yeye alijua udhaifu wako; Yeye alijua mazoea yako. Yeye alijua yote kukuhusu wewe, yale utakayokuwa. Ndiposa, Yeye alipotazama kote kote kwenye ulimwengu mkuu, tuseme, Yeye alisema, “Nilimwona.” Na Yeye alipofanya hayo, kabla chembe ya—ya uhai haijakuwepo bado, ndipo u wa milele pamoja na Mungu. Unapompokea Roho Mtakatifu, basi unakuwa wa milele, kwa sababu una—ulikuwa pamoja na Mungu, u sehemu ya Mungu. Je, mwaweza kuona lile ninalomaanisha? Wewe u wa milele kama Mungu, kwa kuwa tu wewe ni . . .

¹³³ Mimi ni Branham kama baba yangu alivyokuwa Branham, kwa sababu mimi ni damu ya Branham. Mimi ni Branham pamoja na baba yangu, kwa sababu nilizaliwa na baba yangu. Mimi ni Branham pamoja naye. Wewe ni Wood, kwa sababu jina la baba yako ni Wood. Wewe ni Wood kama tu vile Jim Wood alivyo; wewe ni Banks Wood. Amina! Jamani! Wewe ni Neville kwa sababu baba yako alikuwa Neville. Wewe ni Neville kama tu vile yeye alivyokuwa Neville. Utukufu! Sisi tu wa milele kama tu vile Mungu alivyo, kwa sababu sisi ni sehemu ya Mungu, wana wa kiume na wa kike wa Mungu kwa Uzima wa Milele, na hamwezi kuangamia kamwe.

¹³⁴ Si ajabu walipokuwa wakijitayarisha kukata kichwa cha Paulo kule. . . Yeye ilimbidi aiendee njia hiyo ya mauti. Yeye aliandika huo waraka wa mwisho kwa Timotheo, kasema, “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda! Baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, Mhukumu Mwenye Haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kuonekana Kwake.”

Ndipo mauti ilisema, “Naja kukuchukua.”

Yeye alisema, “Uchungu wako uko wapi?”

Kaburi lilisema, “Nitakupata.”

¹³⁵ Kasema, “U wapi ushindi wako?” Lakini yeye alikuwa na kielelezo. Yeye alitazama nyuma kule Kalvari na kusema, “Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” Naam. Jamani, haina budi kuchochea mwamsho; haina budi kufanya hivyo.

¹³⁶ Uzima ni . . . Neno linatoka. Uzima, neno uzima hushika Uzima, na ndani ya mwanadamu kitu fulani hakina budi kupaza sauti.

Mwajua, mtu fulani alisema, “Billy, nini kiwafanyacho watu wasimame na kutupa juu mikono yao au kusema, ‘Bwana asifiwe!’ au ‘Amina!’” Tazama Biblia isemavyo.

¹³⁷ Paulo alisema, “Tukinena kwa lugha zisizojulikana, na asiyefunzwa. . . Yeye anapobarikiwa—kama agebarikiwa, angesemaje, ‘Amina?’” Ona? Yakubidi ujue yale unayonena. Lugha zisizojulikana, isipokuwa ziwe na tafsiri au ufunuo. . .

Ndipo unaweza kusema, “Amina!” kama unaweza kuifahamu. Yeye ajua yale anayonena. Ona?

¹³⁸ Sasa! Ee jamani! Tazama pale siku hiyo maadui walipokuwa wakija kumshambulia Daudi. Naye aliwapa raha zote za mvinyo na—na—minofu ya nyama na mikate. Na—na adui alipokuwa akija, hawakujua la kufanya; nao walikusanyika pale; na Israeli yote ilikusanyika pamoja chini ya tohara. (Sasa, hili liko chini ya tohara ya kale ya Kiyahudi.) Nao waliinua juu mikono yao na kusema, “Mungu, Wewe u Mungu wetu. Umetulinda. Ulimleta nabii Musa, na uliwaleta wana wa Israeli toka Misiri. Uliwaleta kupitia jangwani. Walipokuwa wamelala pale, hakuna hata mmoja aliyegopa ku—kila mtu aliogopa kuwagusa, hakuna mmoja aliyekuwa karibu na urithi wako. Waliogopa sana kufanya hivyo.” Bali walikuwa katika uchache, lakini hamna aliyewagusa. Maana kila kitu kilichowaingilia, kilichomwa pia. Yeye alisema, “Ee, jinsi ulivyo Mungu mkuu. Na sasa, Bwana, kama tumetenda dhambi. . . Wake zetu ndio hawa; watoto wetu hawa; nasi tunateswa wakati huu.” Kasema, “Ee, tufanyeje? Adui yu—yuaja.” Yeye alisema, “Tutafanyeje?”

¹³⁹ Na walipokuwa wakiomba Roho alimshukia mmoja wao pale mkutanoni, naye akatabiri, “BWANA ASEMA HIVI, hamtapigana; tulieni! (Amina) Pitieni njia *fulani* mkawakabili kule.” Na Yeye alisababisha ghasia kati yao, nao wakauana. Naam. Kuchaguliwa tangu awali ukachaguliwa katika Kristo Yesu kabla ulimwengu kuwekwa misingi. Basi.

104. Ulisema kwamba mtu angeishi karibu sana na Mungu hata asitende dhambi hali akiwa hapa duniani. Basi fafana I Yohana 1:8 mpaka 10.

¹⁴⁰ Hebu tuone I Yohana 1:8 mpaka 10. Kama nina wakati zaidi wa kutazama hili. . . Nilikuwa nimepapata; sikuichukua, marafiki. Nili—nilikuwa najaribu ku—kuondoka. . . Vema, nitafungua Yohana baada ya muda mchache. Nita. . . itakuwa upande mwingine wa Waebrania, bila shaka. Vema, I Yohana 1:8 mpaka 10–1 Yohana 1:8 mpaka 10.

Tukisema kwamba. . . hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu.

Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee. . . dhambi zetu, na. . . kutasafisha na udhalimu wote.

Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo wala heno halimo mwetu.

¹⁴¹ Vema sasa, ngoja ndugu yangu mpendwa. Hebu fungua sura ya 3 hapa na kifungu cha 9. Uko katika kurasa ile ile katika Biblia yangu. Kuanzia kifungu cha nane.

Atendaye dhambi ni wa ibilisi; kwa kuwa ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili

Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za ibilisi. (Yale tu ambayo nimekuwa nikinena, ona, Mungu akichagua tungu awali, akikujua wewe.)

Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala havezi kutenda dhambi, kwa sababu ame—ame—kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu.

¹⁴² Hivyo tu ndivyo Neno lisemavyo. Sasa, ukitazama hapa.

Tukisema kwamba . . . hatuuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala neno lake halimo mwetu.

Sasa watu wengine husema, “Vema basi, hapa kuna msichana mdogo mzuri au mvulana mdogo mzuri. Hawakutenda dhambi tangu mwanzo.” Wewe umezaliwa katika dhambi, umeumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo. Unapozaliwa katika ulimwengu huu, wewe u mwongo, u mwizi, wewe u kila kitu kilichoko, wewe wote u dhambi tu, si mwizi, kwa sababu hujaiba. Lakini wewe u—lakini una . . . Wewe si mwongo, kwa sababu hujadanganya. Lakini roho huyo yu ndani yako unapozaliwa, kwa sababu, wewe u na ulimwenguni. Hiyo ndiyo sababu huwezi kuwa na mageuzo, kugeuka; yakubidi ufe na kuzaliwa. Na huwezi kuwa na kuzaliwa bila kusulubiwa. Huwezi kuwa na ufufuo; yakubidi usulubiwe kwa vitu vya ulimwenguni ili upate kufufuka katika Kristo.

¹⁴³ Ukitegemea mawazo yako—yako ya kielimu na hutazaliwa na Roho wa Mungu. Yakubidi usahau, kama Paulo alivyosema, yote aliyowahi kujua, na asijue lo lote kati yenu isipokuwa Kristo Yesu, na kuzaliwa mara ya pili, upya. Ee, kama . . . Hapa . . . Laiti ningeliwaelezeni ninyi. Ona? Ni kuzaliwa kufanyako upya—kiumbe kipya. Lile neno la Kiyunani hapa, kama nilivyokuwa nikilitazama katika kamusi ya Kiyumani majuzi, lile neno *kuzaliwa* maana yake ni “kuumbwa.” Inaposema, “Wewe u kiumbe ki—kipya katika Kristo Yesu,” kuna neno pale, *kiumbe* ni neno *kuumbika*. Wewe ni *kiumbe* kipya, si katika ulimwengu, lakini katika Kristo Yesu. Umekuwa kipya . . .

¹⁴⁴ Sasa, wewe ulikuwa ulimwenguni na kusema, ee, mwajua, mambo ya kufurahisha, nguo nzuri au kitu fulani malidadi. Na . . . ? . . . viko kando. Ona? “Ee, mimi huenda kanisani, hakika. Sitaki kwenda kuzimuni, lakini mwajua . . .” Na macho marembo ya hudhurungi ya msichana, au nywele za ukoka za mvulana, au “Yeye ni m— . . .” Mwajua, kitu fulani au kingine, kitu fulani tu cha kuvutia macho, au yeye ana tamaa mbovu—au kulewa au kitu fulani. Hicho ni ulimwengu; wewe u—wewe u ulimwenguni. Na Biblia ilisema, “Ukiipenda dunia na mambo yaliyomo katika dunia, kumpenda Mungu hakumo ndani yako.” Kwa hivyo ili kuondolea hilo nje yako, yakubidi ufe, sharti ufe, usulubiwe na uzikwe, na ufufuke kiumbe kipya katika Kristo Yesu.

¹⁴⁵ Sasa kabla hujampokea Roho Mtakatifu unaamini *hata* Uzima wa Milele. Lakini huna Uzima wa Milele mpaka utakapompokea Roho Mtakatifu, kwa sababu Yeye ni Uzima wa Milele. Roho Mtakatifu ni Mungu; ni Uzima wa Mungu ndani yako. Ndipo una Uzima wa Milele. Je, wafahamu hilo sasa? Ona? Tazama! Ona? Unaamini *hata*.

¹⁴⁶ Ngoja, hapa kuna jambo nzuri. Ninyi wanawake mniradhi kwa hili kama halikolei (Ona?)...kutaja jambo muhimu. Mwanamke anachukua uhai...Lakini mtoto yule bado hajazaliwa. Lakini ukimtunza mtoto yule vema na kufuata kanuni za maumbile, mtoto yule atazaliwa kawaida. Lakini usipozingatia kila kitu kulingana na kanuni za maumbile, unaachilia pigo kuu, au kugongwa au—au kitu fulani kitendeke, ki—ki—kitamharibu (Ona?); kitamwua mtoto yule kabla hajazaliwa.

¹⁴⁷ Vema, hiyo ndiyo shida. Mapigo yaja toka kwa Shetani. Shetani huchukua mishale ya sumu ya kuzimu na kujaribu kulichubua Kanisa lililo na utungu wa kuzaa mwana. Na kabla hajazaliwa, wanamwua. Lakini ukichukua tu Biblia na kumlisha katika—kumpa chakula cha watoto, mama akila vitamini... Vema, hii ndiyo Vitamini bora niijuayo, Vitamini za kiroho. Ona? Inakujenga.

¹⁴⁸ Sasa, yabidi kanisa liwe likila Vitamini za kiroho; na Vitamini za kiroho zimo mumu humu, Kitabu chote kimejaa hizo. Na yakubidi uwe ukila Vitamini za kiroho, kujifunza, na hilo lamfanya mtoto afikie kuzaliwa. Mwaona ninalomaanisha?

¹⁴⁹ Sasa huyo mtoto mchanga, wakati yeye—yeye—yeye apatapo uhai—yeye—yeye ana uhai, kwa sababu chembechembe ndogo hai zinatikisika na kupiga-piga baada ya karibu miezi mitatu na—au minne. Ndiposa, yeye anapiga-piga na kutikisika lakini yeye bado hajazaliwa. Lakini mara tu aingiapo ulimwenguni, daktari, mama au mtu fulani, anamwinua juu na [Ndugu Branham apiga makofi—Mh.] ampiga kidogo, na “Waaa—a—a!” Pale—pale yeye aanza (ona?), ndiposa yeye anaanza kupumua. Na mara tu yeye apumuapo pumzi ya uhai, ndipo yeye awa nafsi hai.

¹⁵⁰ Na hapo ndipo wakati mwingine...Uko tayari kumpokea Roho Mtakatifu; uko katika utungu; unataka kukombolewa. Wangapi ndani humu wako katika hali hiyo hivi sasa, wakihitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu, wanataka hakika kujua ni nini, wanataka kui—kuingia ndani yake? Nani anahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu? Inueni mikono yenu. Ona? Mko mnaugua, mnataka—mnataka muokolewe. Kile mnachohitaji ni kofi dogo ya Injili, kitu fulani kidogo ambacho [Ndugu Branham apiga makofi—Mh.], na unalia, “Utukufu!” Na inapotendeka...Najua mnadhani mimi nina kichaa, lakini sisi—sisi tulipokea nia ya Kristo ambayo kwa ulimwengu ni kurukwa na akili, haidhuru.

Kitu fulani kinapiga mayowe; Roho huyo anaumuka. Ndipo anaendelea kuingia.

¹⁵¹ Kama nilivyomwambia mtu fulani, ni kama bomba la zamani ambalo halifanyi kazi. Na unaingiza seng'enge ndogo ndani yake na unashikilia seng'enge hii na unachimba, kuchimba, kuchimba. Na kuna bubujiko kubwa la maji yanayojaribu kuvunja. Chimba, uchimbe na uchimbe, lakini unajua kuna kitu fulani juu pale. Unaweza kukigusa; kiko kule mwisho. Ndipo baada ya muda kidogo ukisukume kwa nguvu nyingi mno, na [Ndugu Branham anaiga sauti ya maji yanayobubujika—Mh.] yale maji yakatiririka kwenye mfereji. Hivyo ndivyo ilivyo. Ndipo yale yanaendelea tu kuja. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo. Dhambi ziliufunga mfereji ule. Ninyi—ninyi mliliki nyuma kule na kusema, “Mimi ni mwoga...?...Mwajua...?...Naogopa watu watadhani nilikuwa kule... Roho Mtakatifu.”

¹⁵² Sasa, unaposikia mguso huo mdogo wa Roho... Unamtaka zaidi ya uhai—unamtaka zaidi ya maisha yako wewe mwenyewe. Ni muhimu sana kwako: “Yanibidi nimpokee au nife.” Muda si muda unashikilia kitu fulani. Unawaza. “Hicho ndicho, Bwana.” Unafunua kizibo. Whiu! Hapa yeye aja: Aenda! Jamani! Huru! Ee! lo! Kuna...?...uhai sasa unaokaa pale kasema, “Mungu atukuzwe...?...”

¹⁵³ Petro na wengineo walikuwa nyuma kule wakati wa Pentekoste wakifichana, wakisema, “Chungulieni mlangoni vizuri, chungulieni kama ye yote wa hao Wayahudi anakuja.”

“La. Sioni hata mmoja wao.”

“Vema, tulieni kabisa, kwa sababu nawaambieni, wakifaulu kuja juu humu...?...”

¹⁵⁴ Wao wote walikuwa wameketi pale, na kwa ghafula kukaja sauti toka Mbinguni kama uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi. Ukaanza kuijaza nyumba yote walimokuwa wameketi. Kitu fulani kikaanza kutendeka. Wakatoka mle jengoni; wakafungua wazi milango ile, chini kwenye ngazi wakashuka wakiyumbayumba kama kundi la walevi waliokuwa wame...?...wamejazwa Roho, wakilia tu na kuendelea.

¹⁵⁵ Wao walisema, “Watu hawa wamelewa. Wasikie. Mtazame huyo mwoga akitazamia mlangoni, yule aliyemkana Yesu pale masulubishoni. Kasema, ‘Hata sikumjua Yeye.’ Msichana mdogo alisema, ‘Vema maneno yako yanakuhukumu. Wewe u mmoja wao.’” Kasema, “Yeye alilaani, kasema, ‘Simjui Yeye.’”

¹⁵⁶ Lakini wakati kizibo hicho kilipofunuliwa wakati Roho alipotiririka ndani yake, yeye alisema, “Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu. (Amina!) Mimi ndiye bosi. Na lijueni jambo hili; hawa hawakulewa. (Akilitetea kanisa.) Sivyo mnavyodhani; watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana;

lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli: 'Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu. . . ' Um—m—m, tofauti jinsi gani! Whiu! Lo, najua mwaweza kudhani hili ni jambo la kuogofya, lakini ya—ya—yanibidi niwaonyesheni iliyo Kweli. Kaeni Nayo.

157 Sasa, bila shaka, una Uzima wa Milele.

158 Sasa, kueleza hili. Siku hii. . . "Tukisema kwamba hatukutenda dhambi ('Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu,') twamfanya Mungu kuwa mwongo." Yeye alisema ungetenda dhambi. Ukisema haujatenda dhambi. . . nime. . .

159 "Nilizaliwa katika kanisa la Kibaptisti, kanisa Methodist, kanisa Pentekoste, kanisa Presbiteria; nilizaliwa katika hilo." Hilo halina maana yo yote, yakubidi uzaliwe nje ya hayo tena. Naam. Tukisema hatujatenda dhambi unamfanya Yeye kuwa mwongo. Na Neno, ambalo ni Kweli. . . Wangapi wajua Neno lile ni Kweli? "Hapo mwanzo kulikuwako Neno. . . naye Neno alifanyika mwili, naye Neno. . . " "Baba uwatakase, kwa ile Kweli; Neno Lako ndiyo Kweli." Naye alikuwa lile Neno. Ona? Na Neno, au Kristo hayumo ndani yako. . . Yeye alikuwa lile Neno. Wangapi wajua hilo? Ona? Verna.

160 Tutaisoma hivi basi: "Ukisema hujatenda dhambi, unamfanya Yeye kuwa mwongo na Kristo hayumo ndani yetu." Ona. Ona? Sasa, hilo ni. . . Ona, usemapo ume—kwamba hujatenda dhambi, umekosea. Hauna budi uzaliwe mara ya pili.

161 Sasa, tutafungua hapa katika hiki kifungu kingine. "Yeye. . . Ye yote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, hatendi dhambi, kwa maana. . . "

162 Sasa dhambi ni nini? Nani alisema hilo, mtu fulani? Kutokuamini. Hivyo ndivyo Biblia ilisema. Kuna dhambi moja pekee, na hiyo ni kutokuamini. Naam. "Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumikiwa." Kwa hivyo ninyi—mtu atatenda dhambi.

163 Sasa, ukisema, "Verna sasa, ngoja kidogo. Naamini kwamba huenda hao walimpokea Roho Mtakatifu hivyo siku hizo, lakini siamini ndivyo ilivyo."

164 "Lakini, ndugu, Biblia ilisema, 'Ahadi hii ni kwenu na kwa watoto wenu.'"

"Najua, lakini. . . " Unatenda dhambi. Unatenda dhambi papo hapo. Unakataa kuamini yale Mungu alisema.

"Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele."

165 "Vema, sasa, tumefundishwa kwamba. . . " Sijali umefundishwaje. Biblia ilisema—Yeye alisema, "Na kila neno la mtu liwe uongo na Langu kweli." Vema.

Unasema, "Vema, Yeye—ni Yeye yule hasa, lakini Si. . . Unakusudia ni Yeye yule?"

“Naam, Kanisani akifanya mambo yale yale Yeye aliyofanya alipokuwa hapa.”

¹⁶⁶ “Ee, siwezi kuamini hilo.” Unatenda dhambi. Unatenda dhambi. Na yeye aliyezaliwa na Mungu, na Roho Mtakatifu, hasemi maneno hayo. Naye akisema ana Roho Mtakatifu na asema maneno hayo, hiyo ni ishara kwamba hana Roho Mtakatifu. Sijali yale yeye amefanya. Yeye asipoamini uponyaji wa Kiungu, haamini Nguvu za ufufuo, haamini Roho Mtakatifu anamwagiwa juu yetu sisi kama tu vile ilivyokuwa katika ule wakati wa kwanza, Mungu yule jana, leo, na hata milele, kitu kile mitume walichotenda kimefanyika hivi sasa, kunena kwa lugha, na kufurahi, na mambo haya yote mengineyo; kama hawaamini hayo, yeye hajazaliwa na Mungu. Kwa maana aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi za namna hiyo. Hivyo ndivyo unavyotambua iwapo wamezaliwa na Mungu.

¹⁶⁷ Unamwendea mtu na kusema, “Dk. wa Filosofia, *Fulani na Fulani na fulani*, Padre, Dk., au *Fulani* (ambazo ni nzuri, laiti ngingekuwa nazo, hizo shahada za chuoni), lakini ni kweli kwamba uponyaji wa Kiungu unapaswa kuendelezwa kanisani kama tu mitume walivyofanya?”

“Ee, la, la!” Yeye anayetenda dhambi. Yeye ni asiyeamini. Naam.

¹⁶⁸ Unasema, “Je unaamini tunampokea Roho Mtakatifu kama wao walivyofanya hapa? Nilikuwa nikisoma hapa katika Biblia katika Matendo 2 ambapo ilisema wao walikuwa... na kumwagiwa Roho Mtakatifu, nao walipepesuka kama waliokuwa walevi, nao walienda nje pale na kuongea lugha za watu hao, na mengineyo kama hayo; wakatenda kama watu waliokuwa walevi, na kanisa lilidhani wao wamelewa. Tunapompokea Roho Mtakatifu siku hizi katika kanisa Batisti, Batisti yetu, Methodisti yetu, Presbiteria yetu, lo lote lile, si—sioni tukitenda hivyo.”

“Vema, nakwaambia, mwanangu, hiyo ilikuwa tu ni kwa wale thenashara.” Yeye anatenda dhambi. Yeye hajazaliwa na Roho wa Mungu, kwa sababu Biblia ilisema, “Yeye aliyezaliwa na Roho wa Mungu hakatai kuamini. Yeye ni mwamini, naye hawezi...” Mbona? Mbona? Ee, liko hapa. Yule Hua yuko ndani yake, akimwongoza. Kwa kuwa Roho wa Mungu ako ndani yake, naye hawezi kulikana; yeye hawezi. Kama ni Roho wa Mungu, Mungu hatakana Neno Lake binafsi. Nikikana neno langu mwenyewe, basi ninakuwa mwongo. Na kama—na ukisema una Roho wa Mungu na ukane Neno la Mungu, ni mojawapo ya haya; Mungu ni mwongo au wewe ni mwongo, mmoja wenu. Na Biblia ilisema, “Na kila neno la mtu liwe uongo na Langu Kweli.” Na mtu aliyezaliwa na Roho wa Mungu hawezi kutokubaliana na Neno la Mungu; yambidi yeye asema li—li sahihi. Yeye hawezi kufanya lo lote lingine. Sikiza, hii ni Kweli.

169 Sikia, hebu nisome hili tena.

Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu huo uzao. . .

170 Uzao wa Mungu ni nini? Ile ahadi kwa Ibrahimu—alikuwa na mzao yule ku. . . Nani mzao sasa? Kristo. Je, Kristo ni Mzao wa Mungu? Yeye yu Mzao wa nani kama siye? Vema, vema. Yeye ni Mzao wa Mungu.

171 Ule Uzao wa Mungu unakaa ndani yake. Roho Mtakatifu huja kudumu, si toka mkutano hata mkutano, lakini milele. Sasa, mkitaka kuandika hilo, Andiko lenu kwa haya, Waefeso 4:30: “Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa Yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi.” Ule Uzao wa Mungu wakaa ndani yake, naye hatendi dhambi, kwa sababu yeye amezaliwa na Mungu. Yeye hawezi kutokuamini Neno la Mungu.

172 Sasa, Umwonapo mtu akikataa kukubaliana na Neno la Mungu na kusema, “Ee, hilo lilikuwa la wakati mwingine,” hali ahadi hii ni kwa kila atakaye na aje, kumbuka tu, yeye ni asiyeamini naye si wa Mungu.

Heri tukome hapa, sivyo? Ni saa ngapi? Jamani! Yanibidi—ni—ni—sitaki nirudi hapa tena Jumapili. Hebu nichukue hili upesi, upesi mno. Sivyo? Ni zuri sana. Je hamdhani ni zuri? Ee, Neno la Mungu. Vema.

Ndugu Branham, yambidi mtu afanyaje. . .Hebu nishikilie hilo hadi mwisho, nichukue hili hapa.

105. Tutakuwa na sura gani katika kufufuka kule?

173 Kama tulivyokuwa tulipokuwa tukizikwa. Hakika, kufufuka. . .Hebu—Hebu waza hili. Kitabu hiki kinaanguka sakafuni [Ndugu Branham aangusha kitabu—Mh.], nami nakichukua kitabu hiki, kitabu tofauti, na kukibadilisha. Huo sio ufufuo. *Ufufuo* ni “kuamsha yule yule aliyezikwa.” Je, Yesu alifufuka? Je, walimjua? Je, Yeye alikuwa amesimama pamoja nao, Yesu yule yule? “Basi Yesu huyu aliyechukuliwa juu, atarudi tena katika hali iyo hiyo kama mlivyomwona Yeye akienda.” Ufufuo ni kama tu unapokufa; hivyo ndivyo utakavyofufuka. Unakufa kama mwanadamu katika mwili; unafufuka kama mwanadamu katika mwili. Na Ndivyo ilivyo hasa. Kwa hivyo ufufuo ni vivyo hivyo. Tungechukua masaa mengi kwa hilo, lakini heri tusianze.

106. Eleza Waebrania 4 na 6 (upesi sana sasa, tupate hili upesi sana.) na ulinganishe na Waebrania 10:26—Waebrania 6 na 4. (Samahani, 6:4 na 10:26. Hebu tuone, 10:26 vema, ninayo papa hapa. Ona?)

Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru. Na kukionja. . .kipawa cha mbinguni. Na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,

Na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,

Wakaanguka... baada ya hayo, haiwezekani kwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pill kwa nafsi zao... Na kumfedhehi kwa dhahiri.

¹⁷⁴ Hilo laenda mbele na kueleza lile lita... Sasa tazama. Nilikuwa nalo usiku uliopita. Wangapi walikuwa hapa nilipoeleza hilo? Vema, mwajua ilivyo basi. Ona, ni waamini wakwamia-mpakani.

¹⁷⁵ Wangapi walisoma nyuma kule katika Kumbukumbu La Torati 1, ambako wapelelezi wale waliingia mle na kuonja vitu katika Kanani, ambayo Kanani si mfano wa ule Utawala wa Miaka Elfu. Wangapi wajua hilo? Mwataka kusema, mkono mmoja tu? Junie. Naam. Kanani si mfano wa ule Utawala wa Miaka Elfu, kwa sababu walikuwa na vita, mapigano, mauaji, na kila kitu kinginecho ndani mle Kanani. Iliwakilisha Mtakatifu—Kanani ni mfano wa Roho Mtakatifu. Misri ni ulimwengu waliotoka. Jangwani ndiko ambako walitakasiwa, Kanisa lililoitwa litoke. Kanani ndiko ambako walikaa na Roho Mtakatifu (ona, ona?), kwa sababu bado walikuwa na vita. Na usipoamini una vita, hebu tu pokea Roho Mtakatifu wakati mmoja.

¹⁷⁶ Unafanyaje? Wanafanyaje katika Kanani? Walikuwa wanamiliki haki zao. Utukufu! Walikuwa wanapokea haki zao. Nao hawangemiliki haki zao mpaka walipoingia Kanani. Hawakumiliki cho chote jangwani. Ndipo, walipoingia Kanani, basi walikuwa na haki. Nasi tuna haki. Unapompokea Roho Mtakatifu, umo katika Kanani. Huna budi kupigania; huna budi kupigania kila inchi ya ardhi. Naam, bwana! Hiyo ndiyo sababu watu husema, “Ndugu Branham, niombe leo.” Ingia Kanani mara moja, ndugu, na utatambua mahali pako. Tazama maombi yakianza...? Naam, bwana!

Yeye alisema, “Tazama hapa, Shetani. Hili ni langu! Mimi ni mumiliki wa hiki! Mungu alisema hivyo! Ondoka! (Naam!) Ondoka ardhini mwangu!”

“Ardhini mwako?” Shetani auliza.

“Nina hati ya umilikaji. Ondoka! Kesho nitakupa ilani kwa Roho Mtakatifu.” Yeye ataondoka. Hakika, yampasa afanye hivyo.

¹⁷⁷ Sasa, basi, wale walioonja kipawa cha kimbinguni... Sasa, tazama hapa.

...kama tukifanya dhambi kusudi...(cha 10, hiki ni kifungu cha 26 cha sura ya 10)...kama tukifanya dhambi kusudi baada ya...kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi;

178 Sasa, mahali pamoja ni pale ulipoionja tu, na panapofuata ni ambapo umeupokea na kupata ujuzi wake. Ndipo ukifanya dhambi katika nini? Kutokuamini. . . Sasa, tazama jinsi vyote viwili vinavyosomeka. Ona? “Kama usipoamini kwa makusudi baada ya kupokea ujuzi wa ile kweli. . .” Sasa hebu. . . Hebu kitambo kidogo, hebu niipate hapa.

Kama tutaanguka, kujifanya upya tena. . .

. . . haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, . . . (Kukionja. Ona?) na kufanywa washirika. . . (Ona?). . . wa Roho Mtakatifu.

Na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo.

179 Naye aendelea chini hapa na asema kwamba ukikaa tu kama miiba, kama mvua inyeavyo juu ya nchi nchi; ukikaa tu kama miiba, Roho Mtakatifu alishuka, jamani, unamfurahia tu kama wengine wao; lakini kuhusu kuweka mkono wako juu Yake na kuenda chini pale, kumfanyia Bwana kazi, na kufanya kitu fulani kulihusu, la, la, huwezi kufanya hivyo. Ona? Ndipo hilo laonyesha Roho wa Mungu hayumo ndani yako. Ona? mwishowe unajiangamiza mwenyewe. “Ambao mwisho wao ni kuteketezwa.”

180 Lakini hapa, tusipoamini. . . Sasa dhambi ni nini? Kutokuamini. Kama kitu kile kimefahamika kwako, na unakipa kisogo makusudi na kusema, “Si—si—sitaki uhusiano wo wote nacho,” baada ya wewe kufahamu, hakitabisha moyoni mwako tena. Umekwisha; naam. Ume—umetenda dhambi na kumaliza siku zako za neema. Ona?

Maana, kama tusipoamini kwa kusudi. . . (Sasa katika Biblia yangu nimeiweka alama hapo ambapo ni. . . Kuna herufu “m,” maandishi yaliyo ukingoni hapa, yanasema: dhambi—kutokuamini kwa makusudi. Ona, ona?). . . kwa kusudi baada. . . kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi, (Ukiondoka na kumkataa Mungu kusudi baada ya yote kuwa mema kwako, na Mungu amekupa hayo. . . Ona?)

Bali kuna kuitazamia hukumu kwenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao.

Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma kwa neno la mashahidi wawili au watatu.

. . . Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesahia damu. . . wa agano aliyotakaswa kwako kuwa ni kitu ovyo, . . . na kumfanyia jeuri Roho wa neema? (Ee, lo!)

181 Itakuwaje? Mhubiri, mhudumu, hebu tuchukue. . . Kwa sababu mimi ni mhubiri, hebu tuchukue mhubiri. Akatembea

mpaka humu, akaja humu, akikiri Ukristo, naye aja papa hapa hadi pale ambapo haishi katika zinaa na vitu hivi tena, akiishi maisha mema na masafi, aje humu; neema ya Mungu imekuwa nzuri kwake, ndipo yeye anafikia ujuzi wa Roho Mtakatifu (ona?), anakuja mpaka humu, Mungu amwongoza moja kwa moja mpaka kwa ujuzi wa Roho Mtakatifu, na pale yeye anaiona, lakini yeye asema, “Sasa, ngoja kidogo. Kanisa langu halingekubaliana na hilo. Singelifanya hilo. Wangenifukuza. Lile—lile baraza lingenifukuza. Mkutano wa wahudumu ujao, ningetengwa.” Hakuna tena dhabihu kwa ajili ya dhambi, kwa sababu yeye aliichukua Damu ile ile iliyomtakasa na kumleta umbali huu, kwa ujuzi wa ile Kweli, na kuihesabu kuwa kitu ovyo na kuikanyaga chini ya miguu yake, baada ya Mungu kumwongoza yeye hatua kwa hatua humu kwa Roho Mtakatifu.

¹⁸² Mwasema, “Ee, sasa ngoja kidogo, Ndugu Branham.” Ngoja kidogo: Yule roho wa mpinga Kristo atafanya hilo. Je, uliwahi kutambua vile vichwa viwili vyake? Yuda Isksriote alikuwa nani? Shetani! Biblia ilisema alikuwa mwana wa uharibifu. Uharibifu ni nini? Kuzimu. Yeye ni mwana wa kuzimu, alitoka kuzimuni na akarudi kuzimuni. Naye Yesu Kristo alikuwa Mwana wa Mungu, alitoka Mbinguni, akarudi Mbinguni. Wao wote walipokufa pale misalabani. . . Yuda. . . Je, mlijua Yuda alikufia msalabani? Wangapi wajua hilo? Yeye alikufia mtini. Yesu alikufia msalabani pia. Ungalikatwa; hivyo tu. “Alaaniwe aangikwaye mtini.” Naye alitoka kuzimuni. Basi tazama yale. . . Mradi tu yeye angeweza kujipenyeza aingie kanisani. . . Hicho ndicho kiwango cha juu kabisa awezacho kufikia sasa. Ona jinsi anavyoweza kuwa mdanganyifu, jinsi Yuda alivyokuja? Yeye alikuwa nani? Mweka hazina, ndugu, akifanya kazi kanisani, alimwamini Bwana Yesu Kristo, na ilikuwa tu kama. . . [Ukanda unaisha kabla haujamalizika—Mh.]



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org